# MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mhe. Mwenyekiti,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Manispaa ya Musoma,

## 1.0. UTANGULIZI

Naomba nichukue fursa hii kuwasilisha Rasimu ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha **2020/2021** ikiwa inajumuisha bajeti ya mapato na matumizi katika maeneo ya mishahara, matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Hatua ya kupitisha rasimu hii katika Baraza la Madiwani ni sehemu muhimu ya mchakato wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Mpango na Bajeti hii inajumuisha mapitio ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha **2018/2019**, mapitio ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha **2019/2020** hadi tarehe 31 Desemba, 2019 na maeneo ya kipaumbele kwa mwaka wa fedha **2020/2021.**

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

***Mhe. Mwenyekiti,***

Utekelezaji wa malengo katika bajeti ya mwaka wa fedha **2018/2019** yaliendelea vizuri na utekelezaji wa jumla ulifikia **59.42%.**

***Mhe. Mwenyekiti,***

Katika mwaka wa fedha **2018/2019** Halmashauri ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya **Tzs. 43,518,625,115.91** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato na kiasi kilichokusanywa katika vyanzo vyote ni **Tzs. 25,858,008,114.93** sawa na **59.42%** kama jedwali linavyoonyesha hapa chini:-

**A: MAPATO**

| Maelezo | Makisio | Mapato halisi | % |
|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani | 1,797,271,000.00 | 1,856,386,661.30 | 103.29 |
| Matumizi mengineyo | 663,381,053.83 | 657,642,778.42 | 99.13 |
| Mishahara | 26,769,027,690.00 | 16,071,550,912.03 | 60.04 |
| Miradi ya maendeleo | 14,288,945,372.08 | 7,272,427,763.18 | 50.90 |
| **Jumla** | **43,518,625,115.91** | **25,858,008,114.93** | **59.42** |

**B: MATUMIZI**

| Maelezo | Makisio | Matumizi halisi | % |
|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani | 1,797,271,000.00 | 1,784,386,661.30 | 99.28 |
| Matumizi mengineyo | 663,381,053.83 | 698,019,485.48 | 105.22 |
| Mishahara | 26,769,027,690.00 | 16,071,550,912.03 | 60.04 |
| Miradi ya maendeleo | 14,288,945,372.08 | 7,191,182,633.13 | 50.33 |
| **Jumla** | **43,518,625,115.91** | **25,745,139,691.94** | **59.16** |

Mchanganuo wa mapato ya ndani umeoneshwa kwenye majedwali kama ifuatavyo:-

**Mapato ya ndani (OS)**

| Chanzo | Makisio | Mapato halisi | % |
|---|---|---|---|
| Ushuru wa huduma | 299,100,600.00 | 285,097,188.10 | 95.32 |
| Ushuru wa malazi | 69,062,400.00 | 55,948,438.00 | 81.01 |
| Ada ya maombi ya zabuni | 13,500,000.00 | 14,066,500.00 | 104.20 |
| Ushuru wa masoko | 14,342,000.00 | 40,357,901.00 | 281.40 |
| Kodi ya vibanda | 292,907,296.00 | 278,330,419.24 | 95.02 |
| Leseni za vileo | 15,128,000.00 | 14,273,700.00 | 94.35 |
| Adhabu ya ukiukaji sheria | 8,000,000.00 | 8,642,960.00 | 108.04 |
| Usajili wa pikipiki & bajaji | 16,350,000.00 | 15,236,000.00 | 93.19 |
| Ushuru wa bajaji stendi | 15,065,704.00 | 1,845,500.00 | 12.25 |
| Mapato mengineyo | 3,510,000.00 | 9,386,444.66 | 267.42 |
| Ushuru wa maeneo ya kuoshea magari | 2,520,000.00 | 2,230,000.00 | 88.49 |
| Leseni za biashara | 229,430,000.00 | 233,639,869.50 | 101.83 |
| Ushuru wa machinjio | 48,600,000.00 | 48,566,900.00 | 99.93 |
| Leseni za mitumbwi | 25,000,000.00 | 32,386,000.00 | 129.54 |
| Ushuru wa samaki na dagaa | 141,000,000.00 | 253,115,514.00 | 179.51 |
| Ada ya usafi | 130,542,000.00 | 37,973,221.00 | 29.09 |
| User fee, NHIF & TIKA | 144,036,000.00 | 114,221,927.00 | 79.30 |
| Ada za shule - sekondari | 90,790,000.00 | 213,891,012.80 | 235.59 |
| Ushuru wa madini ujenzi | 40,000,000.00 | 18,301,720.00 | 45.75 |
| Ushuru wa stendi ya magari | 119,718,000.00 | 121,873,400.00 | 101.80 |
| Kodi ya pango la minara ya simu | 29,319,000.00 | 29,974,776.00 | 102.24 |
| Vibali vya ujenzi | 990,000.00 | 4,633,520.00 | 468.03 |
| Ada ya ukodishaji ukumbi | 6,000,000.00 | 9,950,000.00 | 165.83 |
| Ada ya usajili wa Hospitali binafsi | 15,000,000.00 | 11,843,750.00 | 78.96 |
| Ada ya kunyonya maji taka | 27,360,000.00 | 600,000.00 | 2.19 |
| **Jumla (OS)** | **1,797,271,000.00** | **1,856,386,661.30** | **103.29** |

Pamoja na kuwa Halmashauri ilivuka lengo la ukusanyaji wa mapato ya ndani bado kuna vyanzo ambavyo ukusanyaji wake haukufikia 100%. Halmashauri itaendelea kujitahidi kuhakikisha kuwa mapato katika vyanzo ambavyo havikufanya vizuri ukusanyaji wake unatiliwa mkazo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**Ruzuku ya mishahara (PE)**

Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilikisia kupata ruzuku ya mishahara kiasi cha **Tzs. 26,769,027,690.00** na kufikia tarehe 31, Juni 2019 ilikuwa imepokea kiasi cha **Tzs. 16,071,550,912.03** sawa na **60.04% na** kutumia **Tzs. 16,071,550,912.03** sawa na **60.04%**

**Ruzuku ya Matumizi mengineyo (OC)**

**A: MAPATO**

| Kasma | Makisio | Mapato halisi | % |
|---|---|---|---|
| Utawala | 50,114,024.60 | 66,243,314.42 | 132.19 |
| Mifugo na uvuvi | 3,403,500.00 | 850,500.00 | 24.99 |
| Kilimo, umwagiliaji & ushirika | 3,403,500.00 | 5,670,000.00 | 166.59 |
| Elimu msingi | 292,113,029.23 | 274,769,862.00 | 94.06 |
| Afya | 24,000,000.00 | 51,955,102.00 | 216.48 |
| Elimu sekondari | 274,725,000.00 | 244,479,000.00 | 88.99 |
| Maji | 7,860,000.00 | 6,550,000.00 | 83.33 |
| Ujenzi | 7,762,000.00 | 7,125,000.00 | 91.79 |
| **Jumla** | **663,381,053.83** | **657,642,778.42** | **99.13** |

**B: MATUMIZI**

| Kasma | Makisio | Matumizi halisi | % |
|---|---|---|---|
| Utawala | 50,114,024.60 | 56,411,820.50 | 112.57 |
| Mifugo na uvuvi | 3,403,500.00 | 3,313,500.00 | 97.36 |
| Kilimo, umwagiliaji & ushirika | 3,403,500.00 | 2,996,000.00 | 88.03 |
| Elimu msingi | 292,113,029.23 | 254,048,847.29 | 86.97 |
| Afya | 24,000,000.00 | 91,468,660.87 | 381.12 |
| Elimu sekondari | 274,725,000.00 | 275,845,648.18 | 100.41 |
| Maji | 7,860,000.00 | 7,342,550.00 | 93.42 |
| Ujenzi | 7,762,000.00 | 7,592,458.64 | 97.82 |
| **Jumla** | **663,381,053.83** | **699,019,485.48** | **105.37** |

**Miradi ya maendeleo**

**A: MAPATO**

| Chanzo | Makisio | Mapato halisi | % |
|---|---|---|---|
| Health Basket Fund | 35,397,149.00 | 195,120,200.00 | 551.23 |
| CDCF | 36,616,000.00 | 34,616,000.00 | 94.54 |
| Elimu Bila Malipo Elimu (M) | 520,560,000.00 | 435,333,542.67 | 83.63 |
| Elimu Bila Malipo Elimu (S) | 1,226,667,500.00 | 1,476,320,057.51 | 120.35 |
| Global Fund | 34,010,131.48 | 7,081,400.00 | 20.82 |
| AGPAHI | 478,510,200.00 | 245,682,300.00 | 149.97 |
| Ujenzi wa Hospitali ya Hal. | 1,500,000,000.00 | 0 | 0 |
| National Sanitation Prog. | 11,000,000.00 | 21,000,000.00 | 190.91 |
| Sustainable Rural Water Supply | 328,900,000.00 | 0 | 0 |
| TASAF | 100,941,335.00 | 392,289,340.00 | 388.63 |
| EQUIP TZ | 462,575,000.00 | 87,021,952.00 | 18.81 |
| ULGSP | 1,729,656,000.00 | 4,302,962,971.00 | 248.78 |
| **Jumla** | **6,464,833,315.48** | **7,272,427,763.18** | **112.49** |

**B. MATUMIZI**

| Chanzo | Makisio | Matumizi halisi | % |
|---|---|---|---|
| Health Basket Fund | 35,397,149.00 | 189,506,464.50 | 535.37 |
| CDCF | 36,616,000.00 | 34,616,000.00 | 94.54 |
| Elimu Bila Malipo Elimu (M) | 520,560,000.00 | 435,333,542.67 | 83.63 |
| Elimu Bila Malipo Elimu (S) | 1,226,667,500.00 | 1,476,320,057.51 | 120.35 |
| Global Fund | 34,010,131.48 | 7,081,400.00 | 20.82 |
| AGPAHI | 478,510,200.00 | 245,682,300.00 | 51.34 |
| Ujenzi wa Hospitali ya Hal. | 1,500,000,000.00 | 0 | 0 |
| National Sanitation Prog. | 11,000,000.00 | 0 | 0 |
| Sustainable Rural Water Supply | 328,900,000.00 | 20,368,605.45 | 6.19 |
| TASAF | 100,941,335.00 | 392,289,340.00 | 388.63 |
| EQUIP TZ | 462,575,000.00 | 87,021,952.00 | 18.81 |
| ULGSP | 1,729,656,000.00 | 4,302,962,971.00 | 248.78 |
| **Jumla** | **6,464,833,315.48** | **7,191,182,633.13** | **111.24** |

Aidha katika fedha za miradi ya maendeleo zilizotumika kwa mwaka wa fedha wa **2018/2019** kulikuwa na fedha zilizovuka mwaka wa fedha wa **2017/2018** kama inavyoonesha kwenye jedwali lifuatalo:-

| Chanzo | Kiasi cha fedha | Matumizi |
|---|---|---|
| CDCF | 34,062,766.00 | 34,062,766.00 |
| LGDG | 400,000,000.00 | 400,000,000.00 |
| NWSDP | 660,105.90 | 660,105.90 |
| ULGSP | 7,387,797,657.17 | 7,387,797,657.17 |
| TASAF | 496,511.53 | 496,511.53 |
| UNICEF Grant | 1,095,016.00 | 1,095,016.00 |
| **Jumla** | **7,824,112,056.60** | **7,824,112,056.60** |

***Mhe. Mwenyekiti,***

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka **2018/2019** ilipanga kutumia fedha kiasi cha **Tzs. 43,532,338,411.91** ikiwa ni kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo. Hata hivyo hadi tarehe 31 Desemba, 2018 kwa mwaka fedha 2018/2019 Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilikuwa imetumia **Tzs. 12,585,946,666.00** ikiwa ni sawa na **28.91%** ya fedha zilizokisiwa kama jedwali linavyoonyesha hapa chini:-

**B: MATUMIZI**

| MAELEZO | MAKISIO | MATUMIZI | % |
|---|---|---|---|
| Matumizi ya kawaida (mishahara na matumizi mengineyo) | 29,243,393,039.83 | 9,154,229,743.13 | 31.30 |
| Miradi ya maendeleo | 14,288,945,372.08 | 3,431,716,922.87 | 24.02 |
| **Jumla** | **43,532,338,411.91** | **12,585,946,666.00** | **28.91** |

Shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2018/2019 ni kama ifuatavyo:-

**1.0 Utawala**

i. Kusimamia vikao vya Halmashauri

**Vikao vya kisheria ngazi ya Halmashauri**

| Kamati za Kudumu/Baraza | Lengo | Vikao vilivyofanyika | Asilimia ya vikao |
|---|---|---|---|
| | 40 | 40 | 100 |

**Vikao vya kisheria ngazi ya Kata (WDC)**

| Idadi ya kata | Lengo | Vikao vilivyofanyika | Asilimia ya vikao |
|---|---|---|---|
| 16 | 64 | 63 | 98.4 |

**Vikao vya kisheria ngazi ya Mitaa**

| Idadi ya Mitaa | Lengo | Vikao vilivyofanyika | Asilimia ya vikao |
|---|---|---|---|
| 73 | 438 | 408 | 93.1 |

ii. Kushughulikia mashauri ya nidhamu

Katika mwaka wa Fedha 2018/2019, Halmashauri imeendesha Mashauri ya Nidhamu **66** kwa watumishi wake. Hadi kufikia Juni 30, 2019 Mashauri hayo yalikuwa yamefikia hatua mbalimbali kama yanavyosomeka kwenye jedwali hapo chini.

| Watumishi waliopewa adhabu ya Onyo | Kuvuliwa Madaraka | Kushushwa Cheo | Kufukuzwa Kazi | Walioandikiwa hati za mashitaka | Wenye kesi Mahakamani | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 0 | 0 | 1 | 2 | 62 | 0 | 65 |

iii. Kutekeleza zoezi la kusafisha taarifa na uhakiki wa Watumishi na Zoezi la Vitambulisho vya Taifa kupitia mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara (HCMIS LAWSON).

Zoezi la kusafisha taarifa za Kiutumishi na mishahara na Usajili wa Vitambulisho vya Taifa kwa watumishi wa Umma kupitia mfumo wa (HCMIS-LAWSON) lilianza tarehe 24 juni, 2019 na lilikamilika tarehe 06 Julai, 2019. Zoezi hili lilitokana na maagizo ya Serikali kupitia Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa barua yenye **Kumb Na. CP26/205/01"ZZH"/94** ya tarehe **31 Mei, 2019.** Zoezi liliratibiwa na Mkurugenzi wa "Payroll" serikalini na Maafisa kutoka ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Hatua hii ililenga kuwezesha mfumo wa kielekitroniki wa usimamizi wa taarifa za rasilimali watu na mishahara wa sasa kuhamishiwa kwenye mfumo mpya wa (HCMIS) ulioboreshwa ili uweze kutumia **kanzi data (database)** ya mfumo wa vitambulisho vya Taifa (**NIDA),**

ili kupata taarifa zao sahihi zikiwemo za kibaolojia; alama za vidole na cheki namba katika kutambua watumishi wa umma na mambo muhimu yanayohusiana na utumishi wao. Zoezi hili lilihusisha watumishi **1,552** waliopo kwenye orodha ya malipo ya mishahara (payroll) hadi kufikia 30

Juni, 2019. Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imefanikiwa kuhuisha taarifa za watumishi **1,542** kwenye mifumo hii miwili ya HCMIS na NIDA, aidha watumishi **9** hawajasajiliwa kwa sababu ni ajira mpya na taratibu za kukamilisha usajiri wao zinaendelea.

iv. Kuhakiki vyeti vya watumishi
Baraza la Mitihani la Tanzania limeendelea kutoa matokeo ya uhakiki wa vyeti vya watumishi. Bachi ya 12 ya matokeo hayo yalionesha watumishi wawili (02) wa Halmashauri ya Manispaa wamegushi vyeti vya kidato cha nne na sita.

## 2.0 Fedha na Biashara

i. Kukamilisha kazi ya kufunga hesabu za Halmashauri za mwaka **2017/2018** na kuwasilisha hesabu hizo kwa Mkaguzi kwa wakati kama ilivyoelekezwa kwenye kanuni za fedha za Serikali za Mitaa. Katika Hesabu hizo Halmashauri ilipata Hati safi.

ii. Kufanya kazi ya kusimamia na kukusanya mapato kwenye vyanzo vyote vya mapato ya Ndani. Kwa mwaka **2018/2019,** Halmashauri ilikusanya jumla ya **Shs. 1,856,386,661.30** kati ya **Shs.1,797,271,000/=** zilizopangwa, sawa na **103.3%** ya lengo la mwaka. Vyanzo vya mapato vilivyofanya vizuri ni:-
   a) Minara ya simu
   b) Ushuru wa stendi za magari
   c) Ushuru wa Masoko
   d) Kodi za vibanda vya biashara
   e) Ushuru wa Samaki na Dagaa
   f) Ushuru wa Machinjio
   g) Leseni za biashara.

iii. Kuratibu malipo kwenye Idara mbalimbali.

iv. Kuratibu zoezi la kujibu hoja za ukaguzi kama zilivyoibuliwa na Mkaguzi wa Ndani na **CAG.**

v. Kutoa leseni za biashara **3,076** kati ya **3,011** ya lengo la mwaka.

vi. Kutoa leseni za vileo **185** kwati ya **170** ya lengo la mwaka.

vii. Kusimamia ukarabati wa Soko la Mshikamano kwa kuweka kivuli, miundo mbinu ya maji, kukarabati Choo cha Soko na kutengeneza Meza za muda **123.**

## 3.0 Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji

i. Kuratibu na kuandaa Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

ii. Kuandaa mpango kazi (Action plan) wa Halmashauri ya Manispaa ya

Musoma kwa mwaka wa fedha 2019/2020

iii. Kuandaa taarifa mbalimbali kama vile za miradi ya maendeleo kila robo mwaka kwa mwaka wa fedha 2018/2019, taarifa za utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2015.

iv. Kuratibu majibu ya utekelezaji wa maagizo ya viongozi mbalimbali.

v. Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**4.0 Usafishaji na Mazingira**

i. Usafi wa Mazingira kwa kufagia ulifanyika katika barabara zipatazo 289 masoko 6 na stendi 3.

ii. Jumla ya mifereji 209 ya maji ya mvua katika kata 09 ilizibuliwa.

iii. Kiasi cha tani 26,234 za taka ngumu kutoka kwenye kaya, taasisi, makampuni na vizimba zilizolewa, kusafirishwa na kutupwa kwenye dampo.

iv. Ufyekaji nyasi ulifanyika katika maeneo ya wazi 12 na kando kando ya barabara na sehemu za wazi kudhibiti mbu, wadudu na wanyama hatari wadhurifu.

v. Vikundi vitatu (03) vya usafi wa mazingira vilisimamiwa ili kutekeleza majukumu yao ya kufanya usafi katika maeneo yao ya kimkataba.

vi. Elimu kuhusu hifadhi ya mazingira ilitolewa kwenye kongamano la Jumuia ya Wazazi ya CCM Wilaya ya Musoma ambapo zaidi ya watu **50** walishiriki. Aidha vituo **55** vya biashara ndogo na za kati (SMEs) zilitembelewa na kupewa elimu ya mazingira.

vii. Ukaguzi wa mazingira na uratibu wa uandaaji wa maandiko ya kulinda mazingira (EMP) ulifanyika kwa ajili ya vituo **14** vya uchenjuaji dhahabu.

viii. Operesheni ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira ilifanyika katika vilima vya Morembe na eneo la Nyabisare kata ya Bweri na maeneo ya kata za Buhare, Kwangwa na Rwamlimi, kudhibiti uchimbaji na upasuaji holela wa mawe ambapo jumla ya watu **9** walikamatwa na kutozwa faini. Jumla ya Tzs. 850,000.00 zilikusanywa pamoja na mawe kutaifishwa.

ix. Kuiitisha na kusimamia vikao vitatu (03) na wadau wa madini ujenzi kuwapa elimu ya mazingira, ulipaji ushuru na suala la mchakato wa kuanzisha eneo moja la kuchukua madini hayo litakalosimamiwa na Halmashauri (eneo la Mugalanjabo).

x. Kupokea na kushughulikia kero za uchafuzi wa hewa kutokana na vituo vya uchenjuaji vya Madex Co. Ltd na Amago Elution plant katika kata ya Nyakato.

xi. Kituo cha kulelea walemavu cha St. Justine Centre, kata ya Makoko kilitemebelewa na ushauri kuhusu usafi na hifadhi ya mazingira ulitolewa.

xii. Idara ilishiriki kikamilifu katika ziara ya Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Januari Y. Makamba ikiwa ni katika mchakato wa kuutangaza Mlima Mukendo kuwa eneo la Mazingira lindwa.

xiii. Kushirikiana na Mkurugenzi wa MUWASA na timu yake katika kuzuia umwagwaji wa maji taka katika eneo la Nyamitwebiri na kuanza rasmi kutumika kwa malambo ya kutibu maji taka Bweri.

xiv. Vituo 02 vya ufyatuaji tofali vya Mara tofali na cha Mr. Christian Arobogast katika eneo la SIDO vilikaguliwa ambapo jumla ya watu 18 walipewa elimu na maagizo kuhusu utumiaji wa zana kinga (PPE) na usafi wa mazingira.

xv. Miradi mbalimbali ya ujenzi ilitembelewa ili kukagua usimamizi wa masuala ya kimazingira, kiafya na usalama mahala pa kazi (EHS). Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa jengo la mahakama kuu kanda ya Mara katika kata ya Bweri; ofisi za madini katika eneo la Lakeside kata ya Mukendo; Kituo cha Afya Makoko na kituo cha mafuta (petrol station) cha Ketura Micro credit Ltd katika mtaa wa Baruti.

xvi. Usimamizi wa masuala ya kimazingira ulifanyika katika mradi wa ujenzi wa barabara za mjini (km 9.867) kwa kiwango cha lami (Mradi wa ULGSP).

xvii. Usimamizi wa mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM/EIA) ulifanyika katika miradi ya: ujenzi wa ofisi za madini mkoa wa Mara katike kata ya Makoko (lake side), GAPCO vituo 2, Ketura Microcredit Petrol station, Musoma WWTP and sewerage system, Afro Oil, Mahakama kuu Kanda ya Mara na Zahanati ya Marie Stopes Iringo.

xviii. Kusimamia uzingatiaji wa masuala ya mazingira katika kuanzishwa kwa kituo cha uchenjuaji dhahabu cha Mazabu Elution Plant kwa kushirikisha kamati ya Mazingira (WDC) kata ya Nyakato.

xix. Kufanya uratibu na usimamizi wa zoezi la usafi wa mazingira kila jumamosi ya mwisho wa mwezi.

xx. Kuratibu na kuongoza uanzishaji wa chanzo kipya cha madini ujenzi katika eneo la Balima, Mugalanjabo kata ya Buhare ambapo uzinduzi rasmi wa mradi huo ulifanyika tarehe 23/4/2019 na Mgeni rasmi akiwa ni Mhe. Mkuu wa Wilaya.

xxi. Operesheni ya kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki ilifanyika na watu 03 walikamatwa na kutozwa faini ya jumla Tzs. 90,000.00 kwa kukutwa na mifuko hiyo.

xxii. Ukaguzi ulifanyika katika kata ya Kitaji kuhusu utiririshaji wa maji taka ambapo jumla ya watu 4 walitozwa faini ya Tzs. 300,000.00 kwa kosa la kutiririsha majitaka.

xxiii. Kuratibu zoezi la mgawanyo wa vyoo 58 katika maeneo ya shule za Msingi na Sekondari na Vyoo 9 vitakavyojengwa katika maeneo ya wazi ikiwa ni sehemu ya mradi wa mfumo wa majitaka chini ya MUWASA.

xxiv. Kukagua kiwanda cha maji cha Serengeti, kiwanda cha samaki cha MFPL, viwanda 14 vya kuchenjua dhahabu (vat leaching na elution plants), hotel 06, Beach (fukwe zilizoendelezwa) 07, Vituo vya mafuta (petrol stations) 07, Garage 03, viwanda vya mikate 03, Mradi wa Ufugaji samaki wa Jeshi (27 KJ) Lake side na Kiwanda cha nguo cha Mutex.

xxv. Kuzibua mkondo wa maji katika eneo la Nyakato Bondeni ili kuzuia mafuriko.

## 5.0 Afya

i. Kuwapatia huduma za Afya wagonjwa **243,539** waliofika katika vituo vya kutolea huduma za afya kama wagonjwa wa nje. Kati ya hao wagonjwa **19,396** walilazwa katika vituo vya afya Nyasho, Bweri pamoja na hospitali ya rufaa ya mkoa.

ii. Kuwahudumia mama wajawazito **8,718** waliofika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya kliniki, kati yao mama wajawazito **8,093** walijifungua salama katika vituo vyetu vya kutolea huduma.

iii. Huduma ya chanjo kwa watoto walio chini ya miaka mitano ilitolewa ambapo jumla ya watoto **11,941** walipata chanjo.

iv. Vyandarua **6,901** vilitolewa kwa mama wajawazito wa hudhurio la kwanza na watoto **8,981**wenye umri chini ya miaka mitano waliohudhuria kliniki katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuwakinga na mbu waenezao Malaria.

v. Usimamizi elekezi ulifanyika katika vituo vyote **26** vya kutolea huduma za Afya vilivyo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na changamoto zilizoibuliwa zilipatiwa ufumbuzi.

vi. Uhamasishaji wa jamii kuchangia damu ulifanyika ambapo kiasi cha chupa **354** ziliweza kukusanywa na wagonjwa 353 wenye uhitaji wa damu salama waliongezewa damu katika kituo cha Afya Nyasho.

vii. Wazee **417** walipigwa picha na kupewa vitambulisho vya matibabu katika kata **16** na hivyo kufikia idadi ya wazee **4,881** waliopatiwa vitambulisho vya matibabu.

viii. Maandalizi ya kuanza utekelezaji wa bima ya Mfuko wa afya ya jamii iliyoboreshwa yalifanyika. Jumla ya wataalam wa afya **10** na maafisa waandikishaji kutoka katika mitaa **73** wamepatiwa mafunzo na ununuzi wa simu maalumu kwa ajili uandikishaji zimenunuliwa.

ix. Ukaguzi wa majengo mbali mbali 18,025 zikiwemo nyumba za kuishi 17,034 majengo ya biashara 992, Taasisi binafsi na za Umma 78 ulifanyika sambamba na utoaji wa elimu ya Afya na kuhimiza usafi wa mazingira.

x. Kutoa huduma ya mazishi kwa marehemu 16 wasiokuwa na ndugu.

xi. Kukagua na kusimamia usajili wa majengo 248 ili kudhibiti ubora wa chakula, dawa na vipodozi

xii. Ufuatiliaji wa mwenendo wa magonjwa na kutuma taarifa 52 za kuwepo au kutokuwepo kwa magonjwa hatari 23 ya kuambukiza ulifanyika.

xiii. Upimaji wa sampuli 38 za maji (tap water) kuangalia uwepo wa chlorine ulifanyika.

xiv. Kuhimiza na kusimamia kaya 17,034 kuchimba, kujenga na kuboresha vyoo na kuweka vibuyu chirizi.

xv. Kufuatilia na kufanya usimamizi elekezi kwa watumishi katika kata 16 na kutatua kero mbali mbali kuhusu usafi na Afya mazingira.

## 5.1 Hali ya vifo vya wajawazito na watoto wachanga

Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Juni, 2019 wajawazito waliojifungua walikuwa ni **8,327 (Vituoni 8,093, BBA 180, TBA 54**) kati ya hao waliofariki ni 6 **(0.07%)**, vifo hivi vilitokea katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Watoto wachanga waliozaliwa kwa mwaka 2018/2019 ni **8,371** na waliofariki ni **187 (2.2%) Ke 4,270, Me 4,101)** kati ya vifo hivyo 159 vilitokea hospitali ya Mkoa na 28 vilitokea kituo cha Afya Nyasho na Bweri. Vifo vya wajawazito vimepungua ambapo vifo 6 katika mwaka 2018/2019 vimetokea ukilinganisha na vifo 11 vilivyotokea katika mwaka 201/2018. Vifo vya watoto wachanga vimeongezeka kutoka **182** (vifo 43 vilitokea kituo cha afya Nyasho na vifo 139 vilitokea hospitali

ya Mkoa) kwa mwaka 2017/2018 hadi **187** kwa mwaka 2018/2019. Juhudi za kupunguza vifo hivi zinaendelea kwa kuwahimiza akina mama kufika katika vituo vyetu vya afya mapema na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma chini ya uangalizi wa wataalam wenye ujuzi.

## 5.2 Hali ya dawa vituoni

Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, upatikanaji wa dawa ulikuwa mzuri **(98%)** kwani baadhi ya dawa muhimu kama vijiua sumu (antibiotics), dawa za malaria, dawa za maumivu na dawa zingine na baadhi ya vitendanishi na vifaa vya maabara vilipatikana kutoka katika Bohari Kuu ya dawa (MSD).

## 5.3 Utaratibu wa Malipo kwa Ufanisi (Results Based Financing)

Kwa mara ya kwanza Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imeingia katika utaratibu wa malipo kwa ufanisi utakaotekelezwa kwa muda wa mwaka mmoja (Julai 2019 – Juni 2020) ambapo watumishi na wajumbe wa kamati wa kamati za vituo vyetu 10 vya kutolea huduma wamepata mafunzo. Akaunti za vituo vyote zimetumwa wizara ya afya kwa ajili ya kuingiziwa fedha kiasi cha shilingi 10,000,000 kila kimoja kwa ajili ya kufanya maboresho ya miundombinu na vifaa tiba. Baada ya miezi mitatu vituo vitafanyiwa uhakiki na baadae watalipwa kulingana na viwango vya ufanisi.

## 5.4 Miradi ya Maendeleo

### 5.4.1 Ujenzi wa kituo cha afya cha makoko

Mradi huu hadi hapo ulipofikia umegharimu kiasi cha **Tzs. 455,200,000.00**. Mchango wa wananchi katika ujenzi wa kituo hiki ni **Tzs. 700,000.00** pamoja na kazi za kusafisha eneo la ujenzi, kuchimba misingi ya majengo manne na kusomba tripu **20** za mchanga. Mchango wa Halmashauri ya Manispaa hadi sasa ni **Tzs. 54,500,000.00** na mchango wa Serikali Kuu ni **Tzs. 400,000,000.00**. Mradi huu hadi sasa upo kwenye hatua za mwisho za ukamilishaji wa kuweka milango ya ndani ya majengo.

### 5.4.2 Kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Rwamlimi

Katika kuhakikisha tunaboresha huduma za afya ndani ya Manispaa ya Musoma, uboreshaji wa majengo ya kutolea huduma ni moja ya mikakati ya inayotekelezwa ili kurahisisha utoaji wa huduma zenye ubora wa hali

ya juu. Jengo la zahanati ya Rwamlimi limekamilika na huduma imeanza kutolewa. Jumla ya Tzs. **20,000,000.00** zimetumika katika kukamilisha ujenzi wa jengo hilo.

## 6.0 Elimu msingi

i. Kutembelea na kukagua maendeleo ya ufundishaji na ujifinzaji katika shule zote 53 za Halmashauri ya Manispaa.

ii. Kushiriki shughuli maalum ya kusimamia Mtihani wa MOCK Wilaya na Mkoa 2018 na Taifa 2018.

iii. Kusimamia usajili wa wanafunzi wa darasa la IV na VII katika mfumo wa usajili wa Baraza la Mtihani 2018 na 2019.

iv. Kusimamia ukamilishaji wa maboma manne yaliyo kamilishwa na EQUIP Tanzania kwa kushirikiana na TAMISEMI kwa shule ya Kambarage ‘B’ na Kamuyonge ‘B’.

v. Kupokea na Kugawa Vitabu vya Mtaala Mpya kwa Darasa la I hadi IV ambapo vitabu vya kiada vilivyopokelewa ni 19,375, vya Hadithi 9,176 na Miongozo ya ufundishaji kwa walimu Vitabu 912.

vi. Usimamizi na Ufuatiliaji wa vituo vya MEMKWA pamoja na ukaguzi wa ufundishaji kwa kutumia zana.

vii. Kusimamia na kukagua ujenzi wa shule shikizi ya Nyabisare, Bukanga na Nyarusurya. Shule zimefunguliwa kwa darasa la kwanza na darasa la pili kuendelea kusoma.

viii. Kusimamia ujenzi wa madarasa matatu, Bweni moja na uzio wa kuzunguka shule, Ukarabati wa madarasa 29, Bwalo la Chakula, Zahanati, Nyumba za Walimu na kuboresha Miundombinu mingine katika shule ya msingi Mwisenge.

ix. Kusimamia ujenzi na ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 10 kwa shule za Msingi Kiara, Nyarigamba B, Songambele, Rwamilimi A, Rwamlimi B, Nyakato C, Mshikamano A na Kigera B kwa msaada wa EP4R.

x. Kusimamia Uandikishaji wa Darasa la Awali 2019 ambapo Wanafunzi 4,642 (Wavulana 2,337 na Wasichana 2,305) wameandikishwa sawa na asilimia 101 kulingana na maoteo ambayo ni 4,586 (Wavulana 2,217 na Wasichana 2,369).

xi. Kusimamia Uandikishaji wa Darasa la Kwanza kwa mwaka 2019 ambapo Wavulana 2,665 na Wasichana 2,798 jumla 5,463

wameandikishwa sawa na asilimia 114 za maoteo ambayo ni 4,797 (Wavulana 2,357 na Wasichana 2,440).

xii. Kushiriki shughuli maalum ya Uchaguzi wa wanafunzi kuingia kidato cha kwanza 2019 ambapo wanafunzi 3,531 wavulana 1,754 na wasichana 1,777 walifaulu kuingia kidato cha kwanza sawa na asilimia 79.80 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa Taifa wa darasa la Saba 2018.

xiii. Kujaza takwimu kwenye fomu za TSM9, TWM na TSA na kuzituma OR- TAMISEMI pamoja na Baraza la Mitihani kwa shule 53 za Manispaa ya Musoma kupitia mfumo wa BEMIS 2019.

xiv. Kuendesha mafunzo kwa maafisa elimu kata 16 juu ya uingizaji wa taarifa za shule kupitia Mfumo wa KOBO Collection.

xv. Kufuatilia matumizi ya fedha elimu elimu bila malipo zinazotelewa na Serikali kuu kwa shule zote za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

xvi. Kufanya marekebisho ya Ikama ya walimu kwa kuzingatia maelekezo ya EP4R mwaka 2019 kuwabadilishia vituo vya kazi Walimu 45.

xvii. Kushiriki mashindano ya UMITASHUMTA Mkoa yaliyofanyika Wilaya ya Bunda na kisha Kitaifa 2019 Mkoani Mtwara, Wanafunzi 24 kutoka Halmashauri ya Manispaa Musoma walichaguliwa kushiriki mashindano Kitaifa.

## 7.0 Elimu Sekondari

i. Kusimamia matumizi ya fedha za chakula kwa shule tatu 3 za bweni, fedha ya ruzuku (capitation) kwa shule 18 kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia masomo ya sayansi na fidia ya ada kwa ajili ya shughuli za usimamizi na uendeshaji wa shule.

ii. Kufanya ufuatiliaji na kusimamia utendaji na uwajibikaji kazini kwa walimu katika shule za Sekondari 27 katika Halmashauri.

iii. Kupitia maombi ya likizo na kuandaa malipo kwa jumla ya walimu 178 waliokwenda likizo mwezi Disemba, 2018 na mwezi Juni 2019.

iv. Kusimamia mitihani ya Kitaifa kwa kidato cha II, IV na VI ambapo jumla ya watahiniwa 3,443 wa kidato cha pili, 2,197 wa kidato cha nne na watahiniwa 770 wa kidato cha sita walifanya mtihani. Ufaulu wa wanafunzi kwenye mitihani ya Kitaifa kwa kidato cha nne uliongezeka kutoka 69% mwaka 2017 mpaka 72% mwaka 2018 na kwa kidato cha sita ufaulu ulipanda kutoka 97% mwaka 2018 mpaka 99% mwaka 2019.

v. Kusimamia mapokezi na usajiri wa wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2019 ambapo jumla ya wanafunzi 3, 655 sawa na 99.9% walijiunga na kidato cha kwanza kati ya wanafunzi 3,659 waliopangwa na wanafunzi wa kidato cha tano 589 sawa na 75.7% waliripoti kati ya

wanafunzi 778 waliopangwa.

vi. Kuandaa bajeti ya Idara kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

vii. Kuendesha mitihani ya majaribio (Mock) kidato cha IV na VI mwaka 2019 ngazi ya Mkoa.

viii. Kusimamia ujenzi wa madarasa 30 na ukamilishaji wa madarasa 2 katika shule za Sekondari 15. Madarasa 10 yamekamilika na madarasa 20 yako katika hatua mbalimbali.

ix. Kukamilisha ujenzi wa Maabara 5 za Shule za sekondari za Kiara, Makoko, Bweri na Mwisenge.

x. Kusimamia uendeshaji wa michezo ya UMISSETA kuanzia ngazi ya Shule, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa.

xi. Kuandaa takwimu za shule za sekondari kwa mwaka 2019.

xii. Kurekebisha ikama ya walimu kwa kuwabadilishia vituo vya kazi walimu 14.

xiii. Kuandaa orodha ya majina ya majina 136 ya walimu waliostahili kupandishwa cheo ambapo jumla ya walimu 31 wamepandishwa cheo.

## 8.0 Maji

i. Kusimamia ukarabati wa mifumo ya maji safi na majitaka Soko Kuu, Soko la Nyasho, Machinjio ya ng'ombe Bweri Bustani ya Malkia, Ofisi kuu ya Manispaa Musoma, Ofisi ya Afisa Elimu Sekondari, Kituo cha Afya Nyasho, Zahanati ya Makoko, Shule ya Msingi Mukendo, nyumba anayoishi Mkurugenzi, Shule ya Sekondari Mwisenge, Zahanati ya Nyamatare, Zahanati ya Mwisenge, Shule ya msingi Mwisenge na Soko la Sanane.

ii. Kusimamia ujenzi wa matanki ya uvunaji maji ya mvua Buhare Shule ya Msingi na Mshikamano Shule ya Msingi.

iii. Kusimamia ufungaji wa gata katika shule ya Msingi Buhare, Mshikamano, Shule ya Sekondari ya Nyamiongo na kituo cha Afya Bweri pamoja na kubadilisha fishabodi.

iv. Kusimamia kupeleka maji ya bomba katika karo la kuchinjia kuku Soko la Nyasho na Shule ya Msingi Kwangwa

v. Kusimamia ujenzi wa mnara wa tanki la maji ya akiba soko kuu

vi. Kusimamia ufungaji wa mfumo wa maji safi na majitaka katika majengo yanayojegwa katika kituo cha Afya Makoko na ufungaji wa gata.

## 9.0 Maendeleo ya jamii

i. Kuhamasisha uundaji wa vikundi vya uzalishaji mali ambapo vikundi 237 vya uzalishaji mali viliundwa katika kata 16.

ii. Ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo ulifanyika na jumla ya Tzs. 78,016,300.00 zimerejeshwa. Vikundi vya wanawake vimerejesha na Tzs. 68,125,800.00 na vikundi vya vijana vimerejesha 9,890,500.00.

iii. Vikundi 114 vimepatiwa mafunzo elekezi kabla ya kupatiwa mikopo kati

ya hivyo 68 ni vya wanawake,na 46 ni vya vijana.

iv. Kutoa mikopo ya ujasiriamali kwa vikundi ambapo jumla ya Tzs. 143,700,000.00 zimetolewa kwa vikundi 114. Vikundi 68 vya wanawake vimekopeshwa Tzs. 75,700,000.00 na vikundi vya vijana 46 vimekopeshwa Tzs. 68,000,000.00.

v. Uhamasishaji wa jamii kujiunga na mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) katika ngazi ya kaya ulifanyika na kaya 763 zimejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).

vi. Maadhimisho ya sherehe 2 za kitaifa yamefanyika ambazo ni Siku ya Wanawake Duniani na Siku ya Mtoto wa Afrika.

vii. Vikundi 259 vya uzalishaji mali na vya kijamii vimesajiliwa katika kata 16.

viii. Jumla ya kesi 112 zinazohusu ulinzi na usalama wa mtoto zimeshughulikiwa na kutafutiwa ufumbuzi.

ix. Uhamasishaji wa jamii juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU na umuhimu wa upimaji wa VVU umefanyika katika makundi mbalimbali katika kata 5 za mradi wa sauti yetu.

x. Takwimu zilikusanywa na kuandaa taarifa za utekelezaji wa mradi wa sauti yetu kwa kata 5.

xi. Jumla ya watoto 22,462 chini ya miaka 5 sawa na asilimia 94.5 ya walisajiliwa na kupewa vyeti.

xii. WAVIU wamewezeshwa kompyuta mpakato kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu na kutuma taarifa.

**10.0 Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika**

i. Kushiriki katika maonesho ya Kilimo Kitaifa yaliyofanyika kanda ya Ziwa Mashariki mkoani Simiyu ambapo viongozi 10, watumishi 7, wasindikaji 10 na wakulima 5 walishiriki.

ii. Wakulima 8 wa kata za Nyakato 5 na Buhare 3 walipewa mafunzo kuhusu kilimo bora cha vitunguu na nyanya.

iii. Maafisa Ugani 15 walipewa mafunzo kuhusu njia bora za kutoa huduma za ugani kwa wakulima.

iv. Wakulima 4,979 wa mazao mbalimbali katika Kata 16 za Manispaa ya Musoma walitembelewa na kupewa ushauri kuhusu kulima kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo cha mazao wanayolima.

v. Takwimu za bei za vyakula zilichukuliwa kila wiki na kupata wastani wa bei katika mwezi, taarifa ya hali ya chakula kila Mwezi ziliandaliwa na kutumwa Mkoani mara 12.

vi. Wataalamu wa ugani ngazi ya Halmashauri walifuatilia utendaji kazi wa wataalamu wa ugani ngazi ya kata mara kumi kwa mwaka mzima.

vii. Takwimu za kilimo za kila mwezi, robo ya nne na mwaka zilikusanywa na kuingizwa katika mfumo wa "Agricultural Routine data System" (ARDS)- "Web Portal"

viii. Wakulima 12 kutoka kata za Buhare 3, Mwisenge 2, Makoko 4 na Nyasho 3 walipewa mafunzo kuhusu njia mbalimbali za umwagiliaji.

ix. Vikao 11 vya Idara vilifanyika.

x. Usimamizi na ufuatiliaji wa kilimo cha nyanya ndani ya kitalu nyumba ulifanyika mara 23 katika vikundi vya Nyakamitu na Hope revival children's Organization.

xi. Kutoa ushauri na kufanya ufuatiliaji kuhusu utekelezaji wa sheria katika vyama vya ushirika 11 kwa mizunguko 73, Vyama hivyo ni Imara SACCOS Ltd, AIC Nyasho SACCOS Ltd, Musoma Hospital SACCOS Ltd, Mafanikio Mwigobero SACCOS Ltd, Musoma Municipal Council SACCOS Ltd, Musoma SACCOS Ltd, Musoma Dairy SACCOS Ltd, Musoma Urban Teachers SACCOS Ltd, Mara VETA SACCOS Ltd, Kiarano SACCOS Ltd na CHAWASABAMU Multipurpose Co op. Society Ltd. Kiasi cha shilingi 100,000 zilitumika kwa shughuli hii.

xii. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati ya kufufua vyama sinzia ulifanyika katika vyama 10 kwa mizunguko 20 vyama hivyo ni Mkombozi food group Co op. Society Ltd, MUWASA SACCOS Ltd, Kigera SACCOS Ltd , Umoja wa Kahawa SACCOS Ltd, TRA Mara SACCOS Ltd, TANROADS Mara SACCOS Ltd, VIMU SACCOS Ltd, SHAMMAH SACCOS Ltd, Wastaafu SACCOS Ltd TCCIA Musoma SACCOS Ltd. Hali kadhalika ufuatiliaji ulifanyika kwa aliyekua mwenyekiti wa Mara Teachers SACCOS Ltd, chama ambacho ni mfu lakini makato ya baadhi ya waliokuwa wanachama bado yanaendelea kukatwa bila kufahamu yanakokwenda.

xiii. Vikao vya kamati mbalimbali katika vyama vya ushirika 10, mikutano mikuu ya kawaida na usimamizi wa uchaguzi wa viongozi katika vyama 9 vilihudhuriwa na mkutano mkuu maalum 1 kwa lengo la kusomewa taarifa maalum ya uchunguzi na mikutano mikuu maalum 9 katika vyama 6 kwa lengo la kufufua shughuli za vyama hivyo sinzia ambavyo ni Mkombozi food group Co op. Society Ltd, Kigera SACCOS Ltd, Umoja wa Kahawa SACCOS Ltd, VIMU SACCOS Ltd, Wastaafu SACCOS Ltd TCCIA Musoma SACCOS Ltd. Katika jitihadi hizi tumefanikiwa kufufua shughuli za Mkombozi food group Co op. Society Ltd.

xiv. Mafunzo yalitolewa kwa viongozi na wanachama wa vyama vya ushirika 9 kuhusu wajibu wa wanachama na viongozi, taratibu za usimamizi na uongozi katika vyama vya ushirika, udhibiti na ufuatiliaji wa miko**po.** Vyama vilivyohusika ni Imara SACCOS Ltd, AIC Nyasho SACCOS Ltd , Musoma Hospital SACCOS Ltd, Mafanikio Mwigobero SACCOS Ltd , Musoma Municipal Council SACCOS Ltd, Musoma SACCOS Ltd, Musoma Dairy SACCOS Ltd, Musoma Urban Teachers SACCOS Ltd na Mkombozi food group Co op. Society Ltd.

## 11.0 Mifugo na Uvuvi

i. Ununuzi wa chanjo za kichaa cha mbwa (vichupa 160) dozi 1600 pamoja na kutekelaza zoezi kuchanja ulifanyika.
ii. Utambuzi, usajili na upigaji chapa ng'ombe, ambapo ng'ombe 497 walipigwa chapa.
iii. Uimarishaji wa ukaguzi wa afya za mifugo na mazao yake na ukusanyaji wa ushuru wa machinjio ambapo jumla ya mifugo 13,317 iliruhusiwa kuchinjwa na nyama ilikaguliwa na kuruhusiwa kwa matumizi ya binadamu, jumla ya mapato yaliyopatikana ni Tzs. 49,028,200.00.
iv. Kufanya utambuzi wa magonjwa ya mifugo, ufuatiliaji na utoaji wa kinga na tiba kwa mifugo 97,109 katika halmashauri ya manispaa Utekelezaji umefanyika kwa kutumia fedha za wadau kununua dawa kutibia magonjwa.
v. Kutoa huduma ya elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji 6,586 katika Halmashauri ya Manispaa.
vi. Kuingiza taarifa za mifugo na uvuvi kwenye mfumo wa ARDS za kila mwezi taarifa 12, robo taarifa 4 na taarifa ya mwaka 1.
vii. Kusimamia na kufuatilia uboreshaji wa zao la ngozi kwa kufanya ukaguzi wa mabanda 4 ya ngozi, utoaji wa vibali vya kusafirisha ngozi na bidhaa zake katika Halmashauri yetu.
viii. Kufanya doria 34 ndani na nje ya Ziwa Victoria ambapo jumla ya nyavu haramu 1,197 zilikamatwa. Elimu juu ya uvuvi endelevu ilitolewa kwa wadau 814 walioko kwenye mialo na mabwawa ya ufugaji wa samaki.
ix. Kutoa leseni za mitumbwi 172 na ukusanyaji wa mapato ambapo Tzs. 37,346,150.00 zilikusanywa.
x. Kutoa elimu juu ya ufugaji bora wa samaki kwa wafugaji 814 wa samaki.
xi. Uboreshaji wa mwalo wa Nyarusurya kwa ajili ya wafanyabiashara waliohamishwa mwalo wa Mwigobero ulianza na kazi haijakamilika.

## 12.0 Mipango miji na Ardhi

### (a) Sehemu ya Ardhi

i. Jumla ya hati **499** zimeandaliwa na kupelekwa ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi kanda kwa hatua zaidi za uidhinishwaji wake.
ii. Jumla ya **Tzs. 426,227,209.38** zimekusanywa kama kodi ya ardhi kati ya lengo la Tzs. **1,000,000,000.00**
iii. Usuluhishi wa Migogoro **193** ya Wananchi umefanyika.

### (b) Sehemu ya Upimaji na Ramani.

i. Jumla ya Viwanja **4,100** vimeanishwa na kupimwa katika maeneo mbalimbali ambayo ni Kiara idadi ya viwanja 856, Buhare-Mugharanjabho idadi ya viwanja 980, Mshikamano idadi ya viwanja

1250 na Nyakato idadi ya viwanja 1014. Katika lengo la upimaji wa **viwanja 3,000**

ii. Jumla ya viwanja **1,480** vimeainishwa ili kuandaa michoro ya Mipango Miji katika Mtaa wa Bukoba viwanja **1,000**, Mwiyale "A" viwanja 250 na Kwangwa "A" viwanja 230.

iii. Jumla ya Ramani ndogo za **Hati 600** zimeandaliwa kati ya lengo la kuandaa ramani ndogo (deed plan) **6,000.**

**(c) Sehemu ya Uthamini.**

i. Maeneo **2** (**Balima na Makoko Jeshini**) yaliyotwaaliwa kwa masilahi ya umma yamefanyiwa uthamini kwa ajili ya fidia ambapo Balima ni wananchi **86** na Makoko jeshini 27KJ ni wananchi **65**.

ii. Jumla ya wananchi **5** wamefanyiwa uthamini kwa ajili ya fidia kati ya lengo la wananchi 8.

iii. Jumla ya viwanja **73** vimefanyiwa uthamini ajili ya kuhamisha miliki; kati ya lengo la viwanja **60.**

iv. Jumla ya viwanja **14** vimefanyiwa uthamini kwa ajili ya kuhuisha hati miliki ambazo muda wake umekwisha; kati ya lengo la viwanja **12.**

v. Jumla ya viwanja **9** vimefanyiwa uthamini kwa ajili ya dhamana kati ya lengo la viwanja **20.** Pia mali za kudumu za taasisi **2** zimefanyiwa uthamini kwa ajili ya utoaji wa taarifa za kifedha (Financial reporting).

**(d) Sehemu ya Mipango Miji.**

i. Michoro **49** imeandaliwa maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Musoma.

ii. Jumla ya vibali 108 vya ujenzi vimetolewa katika maeneo yasiyopimwa (Squatter area).

## 13.0 Ujenzi

i. Kusimamia ubora wa kazi za ujenzi wa majengo katika Taasisi zinazosimamiwa na Halmashauri ya Manispaa kama vile ujenzi wa kituo cha afya Makoko, ukarabati wa shule ya msingi Mwisenge, ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari.

ii. Idara ilisimamia ufunguzi wa barabara yenye urefu wa km 2.8 iendayo katika eneo la kuchimba madini ujenzi Buhare – Mugaranjabo (Balima) pamoja na ujenzi wa Kalvati moja, kuweka changarawe katika pande mbili zinazopakana na Kalvati na baadae kusimamia ujenzi wa kibanda cha Mkatisha ushuru. Shughuli zote hizi ziligharimu fedha kiasi cha **Tzs. 45,552,300.00.**

iii. Idara kwa mwaka 2018 – 2019 ilipokea jumla ya ramani sabini (70) kwa ajili ya kupata vibali vya ujenzi, aidha vibali hivyo tayari vimeshatolewa kwa wahusika kuendelea na ujenzi.

iv. Kuendelea kusimamia ujenzi wa barabara za lami Mjini kwa kiwango cha lami zenye jumla ya km 10.023 ambapo hadi kufikia tarehe 30/06/2019 shughuli zifuatazo zimetekelezwa katika hizo barabara ni kama ifuatavyo:-.

**Awamu ya kwanza:** *Barabara ya Mutex-Buhare jumla ya Km 4.6*

- Kujenga mifereji na Makalvati katika maeneo mbalimbali ya barabara. Jumla ya kalvati 11 na mifereji karibu mita 2,600 zilijengwa na kukamilika.
- Kazi ya kuimarisha tabaka la barabara kwa changarawe (Improved sub grade) yenye ubora wa G3, G7 na G15.
- Kuweka tabaka la C1 katika barabara.
- Kuweka tabaka la CRR Barabarani.

**Awamu ya pili:** *Barabara za mjini km 4.246*

- Kujenga mifereji na Makalvati katika maeneo mbalimbali ya barabara. Jumla ya kalvati 15 na mifereji karibu mita 3,600 zilijengwa na kukamilika.
- Kazi ya kuimarisha tabaka la barabara kwa changarawe (Improved sub grade) yenye ubora wa G3, G7 na G15.
- Kuweka tabaka la CM barabarani.
- Kuweka tabaka la CRS Barabarani.
- Kuweka tabaka la lami km 2.6 barabarani.
- Kuweka lami nyepesi (Prime coat) km 1.345.

**Awamu ya tatu:** *Barabara za Nyasho sokoni Km 1.1*

- Kuimarisha kitako cha barabara (Road bed preparation).
- Kujenga Kalvati 2 kalvati 15

Hadi kufikia Juni 30, 2019 Halmashauri ilikuwa imelipa jumla ya **Tzs. 6,917,313,270** kwa Mkandarasi na **Tzs. 964,920,000.00** kwa Mhandisi Mshauri wa kusimamia kazi hiyo na utekelezaji wa mradi ukiwa umefikia asilimia 73.

## 14.0 Kitengo cha Teknolojia, Habari, Mawasiliano na uhusiano

i. Uingizaji na uhuishaji wa taarifa katika tovuti umefanyika ambapo jumla ya taarifa mpya 106 zimewekwa katika tovuti. Uandishi wa makala, Uhariri wa picha za mnato na video, Ukusanyaji wa taarifa muhimu za idara mbalimbali kwa ajili ya kuziingiza kwenye tovuti ya Halmashauri ulifanyika.

ii. Uchukuaji na uhifadhi wa matukio muhimu yaliyofanyika katika Manispaa ikiwa ni uchukuaji wa picha za mnato, video na sauti. Jumla ya picha za mnato 932 na video 27 zilichukuliwa.

iii. Ufungaji wa mfumo wa mapato (GoT-HOMIS) katika vituo vya Nyasho na Bweri pamoja na zahanati za Mwisenge, Nyakato, Buhare na Makoko. Zoezi la ufungaji mfumo kwenye vituo vingine vya Afya na Zahanati linaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha zilizopangwa kwa ajili ya kazi hiyo.

iv. Jumla ya malalamiko 106 yalipokelewa na kupelekwa idara husika kwa ajili ya utatuzi ambapo kati ya malalamiko 106 yaliyopokelewa malalamiko 97 yamekamilika na lalamiko 9 liko katika hatua mbalimbali za utatuzi.

v. Usimikaji wa kamera maalum (CCTV CAMERA) katika kituo cha Mabasi Bweri ili kuongeza ufanisi wa kituo na udhibiti wa mapato.

vi. Kitengo kilihakikisha mifumo ya GSPP, PLANREP, FFARS, TASAF, EPICOR, HCMIS, BEMIS, GoT-HoMIS, LGRCIS na TSA inakuwa salama na inafanya kazi ipasavyo.

vii. Kitengo kwa kushirikiana na idara ya Fedha na Biashara kilihakikisha kuwa vifaa vinavyotumika kukusanya mapato (POS) vinakuwa salama na vinafanya kazi ipasavyo, hii ikiwa ni pamoja na kuvikagua mara kwa mara na kuhakikisha taarifa zote zimetumwa kwenye mfumo wa mapato (LGRCIS).

viii. Utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA katika idara mbalimbali ulifanyika ili kuhakikisha usalama na utendaji kazi wake unakuwa katika hali nzuri ambapo jumla ya vifaa 101 vilitengenezwa.

ix. Usajili wa vifaa vyote vya TEHAMA vinavyomilikiwa na ofisi ili kuboresha takwimu na udhibiti wa matumizi ya mtandao ulifanyika.

## 15.0 Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi

i. Kusimamia ununuzi wa vifaa na bidhaa, huduma zisizo za kitaalam, huduma za ushauri wa kitaalam na kazi mbalimbali za miradi wenye gharama ya Tzs. 5,177,498,050.00.

ii. Kuitisha vikao vya PMU na Bodi ya Zabuni ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, Bodi ya Zabuni ilikaa vikao vya kawaida 6 na Vikao 5 vya maamuzi kwa njia ya mzunguko (circular Resolution). Aidha kitengo cha Ununuzi na Ugavi kilifanya vikao 11 ikiwa ni kwa ajili ya ufunguzi wa zabuni mbalimbali na upitiaji wa taarifa mbalimbali zinazohusiana na ununuzi.

iii. Kitengo kiliandaa Mpango wa Ununuzi wa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa kuzingatia sheria ya ununuzi na.7 ya mwaka 2011.

## 16.0 Kitengo cha Sheria na Usalama

i. Kuendelea kusimamia kesi za madai **31** ambazo ziko katika mahakama mbalimbali (Mahakama Kuu ya Tanzania – Mwanza, Mahakama ya Wilaya – Musoma, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya – Musoma,

Mahakama ya Hakimu Mkazi – Musoma na Tume ya Usuluhishi na uamuzi wa Migogoro ya kazi (CMA)).

ii. Kuendelea kutoa ushauri kwa lengo la kumaliza kesi kwa kuzingatia misingi ya haki na ushauri huo ulilenga kuzuia hasara zaidi zinazoweza kujitokeza upande wa Halmashauri.

iii. Kuondoa wafanyabiashara katika maeneo yasiyoruhusiwa maeneo ya Manota kata ya Mwigobero, Stendi ya zamani, Serengeti, Bustani ya Malkia, Uhuru, Serengeti na Rutiginga.

iv. Kukamata mifugo iliyokuwa inazurura mjini na kutoza wamiliki faini ikiwa ni pamoja na kutoa onyo kwa wamiliki wa mifugo hiyo. Ng'ombe **180**, mbuzi **80** na kondoo **7** walikamatwa.

v. Kuandaa na kutunga marekebisho ya sheria ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

vi. Kukamilisha na kuunda upya mabaraza ya kata 16 zilizopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

vii. Kupitia mikataba yote ambayo Halmashauri ni mhusika.

## 17.0 Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

i. Kufanya ukaguzi kwa ajili ya kufanya tathimini kwa shughuli zilizofanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 kwa kufanya ukaguzi wa nyaraka (Transaction Audit) na ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Lengo ukaguzi likiwa ni kulinganisha ufanisi wa Halmashauri na malengo ya serikali kwa madhumuni ya kuongeza umakini katika maeneo yasiyofanya vizuri, uwajibikaji na kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inafikiwa katika matumizi ya rasilimali za serikali.

ii. Kufuatilia ili kujiridhisha kama mfumo wa udhibiti wa ndani unafanya kazi na kufuatilia hoja za nyuma.

iii. Kuandaa taarifa za ukaguzi wa ndani kwa kila robo mwaka.

## 18.0 Kitengo cha Nyuki

Shughuli zilizotekelezwa ni zifuatazo:-

i. Kuhamasisha vikundi vinne (Community Alive, Eliama Family, Nyamutitana Taro) vilivyopo kukagua mizinga ya nyuki na kuifanyia ukarabati mizinga mibovu.

ii. Kutafuta makundi ya nyuki kwa mizinga isiyokuwa na nyuki.

iii. Kuvuna asali kwa mizinga iliyokuwa na asali.

## 19.0 Kitengo cha uchaguzi

Hakuna shughuli iliyotekelezwa na kitengo cha uchaguzi.

**Mafanikio**

Katika kutekeleza mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 mafanikio yafuatayo yalipatikana:-

i. Ukusanyaji wa mapato ya ndani ulifikia asilimia 103.29.
ii. Halmashauri ilipata Hati safi ya mahesabu.
iii. Uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali ulifikia 101 na darasa la kwanza ulifikia asilimia 114.
iv. Halmashauri ilikamilisha vyumba vya madarasa 13 na ukarabati wa matundu ya vyoo 50 katika shule za msingi.
v. Halmashauri imeendelea kuwa na kiwango cha juu cha chanjo zaidi ya 100%.
vi. Kuongeza idadi ya vituo vya afya kutoka viwili (2) hadi vitatu (3) kwa kujenga Kituo cha Afya cha Makoko.
vii. Kuongeza idadi ya zahanati za serikali kutoka saba (7) hadi nane (8) kwa kukamilisha zahanati ya Rwamlimi.
viii. Kuongeza urefu wa barabara za lami kwa km. 8.85.
ix. Halmashauri ilikuwa mshindi wa kwanza kitaifa na kutoa mkulima mshindi wa kwanza katika maonesho ya kilimo yaliyofanyika kitaifa mkoani Simiyu.

Halmashauri katika kutekeleza shughuli mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

| Na. | Changamoto | Suluhisho |
|---|---|---|
| 1. | Upungufu wa watumishi hususani katika Idara ya Afya, Elimu Msingi na Sekondari | Kufuatilia vibali vya ajira na kuajiri watumishi |
| 2. | Kutotolewa kwa fedha kwa ajili ya utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na upungufu wa fedha za uendeshaji wa Halmashauri. | Kuendelea kuomba Serikali kutoa fedha kwa mujibu wa mpango kazi wa Halmashauri. |
| 3. | Upungufu wa vitendea kazi. | Kununua vitendea kazi |

## 3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

***Mhe. Mwenyekiti,***

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya **Tzs. 21,844,325,813.68** na hadi tarehe 31 Desemba, 2019 kiasi ilichokusanya katika vyanzo vyote ni **Tzs. 9,988,189,820.42** sawa na **45.72%** kama jedwali linavyoonyesha hapa chini:-

**A: MAPATO**

| MAELEZO | MAKISIO | MAPATO | % |
|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani | 2,131,421,000.00 | 967,552,242.89 | 45.39 |
| Matumizi mengineyo | 703,619,000.00 | 449,353,540.00 | 63.86 |
| Mishahara | 16,427,703,000.00 | 7,989,342,500.00 | 48.63 |
| Miradi ya maendeleo | 2,581,582,813.00 | 581,941,537.53 | 22.54 |
| Wahisani | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **21,844,325,813.00** | **9,988,189,820.42** | **45.72** |

Mchanganuo wa mapato ya ndani ni kama ifuatavyo:-

**Mapato ya ndani (OS)**

| NA | CHANZO | MAKISIO |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa machinjio | 48,600,000.00 |
| 2 | Ushuru wa stendi ya mabasi na taxi | 120,960,000.00 |
| 3 | Ushuru wa huduma | 316,350,000.00 |
| 4 | Leseni za vileo | 15,128,000.00 |
| 5 | Ada ya usajili wa magari mdogo | 16,350,000.00 |
| 6 | Ushuru wa samaki na dagaa | 170,040,000.00 |
| 7 | Kodi ya vibanda | 252,227,297.04 |
| 8 | Mapato mengineyo (ushuru wa vyoo & bafu) | 50,454,000.00 |
| 9 | Ada ya maombi ya zabuni | 13,500,000.00 |
| 10 | Ada ya nyumba za kulala wageni | 69,062,400.00 |
| 11 | Ada ya kunyonya maji taka | 27,360,000.00 |
| 12 | Leseni za biashara | 240,080,000.00 |
| 13 | TIKA/NHIF/USER FEE | 143,551,304.00 |
| 14 | Ada ya usajili wa vibali vya maduka ya dawa na chakula | 12,000,000.00 |
| 15 | Ada ya usajili wa Hospitali bianafsi | 15,000,000.00 |
| 16 | Ushuru wa masoko na gulio | 71,136,000.00 |
| 17 | Ada ya usajili wa vyombo vya majini | 25,000,000.00 |
| 18 | Ushuru wa maeneo ya kuoshea magari | 2,520,000.00 |
| 19 | Adhabu ya ukiukwaji wa sheria | 20,000,000.00 |
| 20 | Ada ya vibali vya ujenzi | 6,000,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 21 | Ukodishaji ukumbi | 6,000,000.00 |
| 22 | Ushuru wa minara ya simu | 29,400,000.00 |
| 23 | Ada za shule za sekondari (kidato cha V & VI) | 90,160,000.00 |
| 24 | Ushuru wa madini ujenzi | 240,000,000.00 |
| 25 | Ada ya kuzoa taka | 130,542,000.00 |
| | **Jumla** | **2,131,421,001.04** |

***Mhe. Mwenyekiti,***
Mpaka kufikia tarehe 31 Desemba, 2019 Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilikua imekusanya kiasi cha Tzs. 967,552,242.89 sawa na asilimia 45.39 ya mapato ya ndani.

***Mhe. Mwenyekiti,***
Katika mwaka wa fedha **2019/2020** Halmashauri ilikisia kutumia **Tzs. 706,867,000.00** kati ya **Tzs. 2,131,421,001.04** zilizokisiwa kukusanya kama mapato ya ndani kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

**Ruzuku ya mishahara (PE)**
Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikisia kupata ruzuku ya mishahara kiasi cha **Tzs. 16,427,703,000.00** na kufikia tarehe 31, Desemba 2019 ilikuwa imepokea kiasi cha **Tzs. 7,989,342,500.00** sawa na asilimia **48.63.**

**Ruzuku ya Matumizi mengineyo (OC)**

| Kasma | Makisio | Mapato halisi | % |
|---|---|---|---|
| Utawala | 59,063,000.00 | 29,923,041.25 | 50.66 |
| Mifugo na uvuvi | 3,403,500.00 | 929,490.48 | 27.31 |
| Kilimo, umwagiliaji & ushirika | 3,403,500.00 | 944,900.00 | 27.76 |
| Elimu msingi | 292,113,029.23 | 196,865,557.78 | 67.39 |
| Afya | 69,928,000.00 | 50,344,600.00 | 71.99 |
| Elimu sekondari | 267,945,970.77 | 166,984,970.62 | 62.32 |
| Ujenzi | 7,762,000.00 | 3,360,979.87 | 43.30 |
| **Jumla** | **703,619,000.83** | **449,353,540.00** | **63.86** |

**Miradi ya maendeleo**

| Chanzo | Makisio | Mapato halisi | % |
|---|---|---|---|
| CDCF | 36,616,000.00 | 36,616,000.00 | 100 |
| Elimu Bila Malipo | 2,091,461,000.00 | 547,325,537.53 | 26.07 |
| PEDP | 50,000,000.00 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2,091,461,000.00** | **581,941,537.53** | **27.82** |

***Mhe. Mwenyekiti,***
Katika fedha za miradi ya maendeleo zinazotarjiwa kutumika kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kuna fedha zilizovuka mwaka 2018/2019 kama inavyoonesha kwenye jedwali lifuatalo:-

| Chanzo | Kiasi cha fedha |
|---|---|
| BASKET FUND | 42,012,914.00 |
| AGPAH | 100,021,301.00 |
| GLOBAL FUND | 7,036,333.82 |
| ULGSP | 7,958,802,212.83 |
| EQUIP - T | 140,771,769.38 |
| P4R | 281,699.39 |
| OWN SOURCE DEV | 100,482,822.66 |
| **Jumla** | **8,377,318,357.97** |

***Mhe. Mwenyekiti,***
Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka **2019/2020** ilipanga kutumia fedha kiasi cha **Tzs. 21,844,325,813.68** ikiwa ni kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo. Hata hivyo hadi tarehe 31 Desemba, 2019 kwa mwaka fedha 2019/2020 Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilikuwa imetumia **Tzs. 9,704,035,749.53** ikiwa ni sawa na **44.42%** ya fedha zilizokisiwa kama jedwali linavyoonyesha hapa chini:-

**B: MATUMIZI**

| MAELEZO | MAKISIO | MATUMIZI | % |
|---|---|---|---|
| Matumizi ya kawaida (mishahara na matumizi mengineyo) | 19,752,864,813.68 | 9,122,094,212.00 | 46.18 |
| Miradi ya maendeleo | 2,091,461,000.00 | 581,941,537.53 | 27.82 |
| **Jumla** | **21,844,325,813.68** | **9,704,035,749.53** | **44.42** |

***Mhe. Mwenyekiti,***
Kati ya fedha kiasi cha **Tzs. 967,552,242.89** za mapato ya ndani zilizokusanywa na Halmashauri hadi tarehe **31 Desemba, 2019** kiasi cha **Tzs. 237,200,000.00** kati ya **Tzs. 706,867,000.00** zilizokisiwa zilitumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Katika Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha **2019/2020** Halmashauri ilikuwa na malengo **138** yaliyopangwa kutekelezwa na idara na vitengo, hata hivyo Halmashauri hadi tarehe 31 Desemba imefanikiwa kutekeleza sehemu ya malengo **68.** Miongoni mwa shughuli ambazo zimetekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida ni pamoja na:-

***Utawala***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kusimamia utendaji wa watumishi.
ii. Kuendesha vikao vya Kamati za kudumu na Baraza la Manispaa na kulipa stahili za waheshimiwa madiwani za kila mwezi.
iii. Kufuatilia na kuratibu vikao vya kata na mikutano ya mitaa

Shughuli zote zilizotekelezwa zilizogharimu **Tzs. 350,531,420.54.**

***Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kufuatilia utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019.
ii. Kuanza maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2019/2020.
iii. Kuandaa taarifa mbalimbali kwa robo zote 2 za mwaka.

Shughuli zote zilizotekelezwa zilizogharimu **Tzs. 5,645,000.00**

***Fedha na Biashara***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ulifanyika.
ii. Kuandaa malipo mbalimbali na kuyalipa.
iii. Kuandaa taarifa za kila mwezi na za kila robo mwaka ili kukidhi matakwa ya kanuni za fedha.
iv. Kukamilisha zoezi la kufunga mahesabu ya mwaka wa fedha 2017/2018 na kuyawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati.
v. Kuhamasisha wafanyabiashara ndogondogo kutumia masoko yaliyo rasmi kwa lengo la kuboresha usafi wa mazingira na kukusanya ushuru wa masoko.
vi. Kusimamia masoko na magulio 6.

Shughuli zote zilizotekelezwa zilizogharimu **Tzs. 54,640,276.35.**

***Afya na ustawi wa jamii***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kutoa huduma za Afya kwa wagonjwa **54,136** waliofika katika vituo vya kutolea huduma za afya kupata matibabu kama wagonjwa wa nje. Kati ya hao wagonjwa **4,559** walilazwa na wagonjwa **869** walipewa rufaa kwenda Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwa matibabu zaidi.
ii. Kuwahudumia mama wajawazito **2,136** waliofika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya kliniki, mama wajawazito **2,169**

walijifungua salama katika vituo vyetu ingawa akina mama **6** walifanyiwa upasuaji katika kituo cha afya Nyasho.

iii. Kutoa huduma ya chanjo kwa watoto walio chini ya miaka mitano ambapo watoto **2,460** walipatiwa huduma hiyo.

iv. Kugawa vyandarua kwa mama wajawazito **1,740** wa hudhurio la kwanza na watoto chini ya miaka mitano **2,537** waliohudhuria kliniki katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuwakinga na mbu waenezao Malaria.

v. Kufanya usimamizi elekezi katika vituo **27** vya kutolea huduma za Afya vilivyo ndani ya Halmashauri ya Manispaa na changamoto zilizoibuliwa zimepatiwa ufumbuzi.

vi. Kufanya uhamasishaji wa jamii kuchangia damu na kiasi cha chupa **194** zimeweza kukusanywa na wagonjwa **86** wenye uhitaji wa damu salama waliongezewa damu katika kituo cha Afya Nyasho.

vii. Kuwapiga picha wazee **45** katika kata **16** kwa ajili ya kuwapatia vitambulisho vya matibabu katika robo hii na hivyo kufikia idadi ya wazee **4,639** waliopatiwa vitambulisho vya matibabu bure.

viii. Uhamasishaji wa jamii kujiunga na mfuko wa Afya ya jamii (CHF) umefanyika ambapo kaya **200** zimejiunga na mfuko huu kwa robo hii katika vituo vya afya **2** na zahanati **8,** na hivyo kufikisha kaya **5,007** zilizojiunga na CHF kati ya kaya **27,060 (18.5%)**

ix. Kuendelea na ujenzi wa kituo cha Afya kipya cha Makoko unaoendelea kwa kushirikiana na kamati za ujenzi ambapo majengo yote matano (Jengo la Maabara, Jengo la wazazi, Jengo la Upasuaji, Jengo la Kufulia na Nyumba ya mtumishi ) yapo kwenye hatua ya umaliziaji.

x. Kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Rwamlimi na tayari huduma zimehamia katika jengo jipya na huduma zinaendelea kutolewa.

xi. Kufanya maandalizi ya mipango ya Afya, ambapo mipango ya vituo vya afya 2 na zahanati 8 iliweza kuandaliwa na baadaye kuunganishwa katika mpango kamambe wa afya kwa ajili ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

xii. Kutoa huduma ya mazishi kwa marehemu 9 wasiokuwa na ndugu .

xiii. Kukusanya sampuli 9 za maji kuhakiki usalama na ubora wa maji.

xiv. Kufanya ukaguzi katika Mitaa 73 na kuhimiza jamii kuchukua hatua ya kuweka usafi wa mazingira na kuangamiza mazalio 5 ya mbu katika maeneo yao.

xv. Kukagua na kusimamia usajili wa majengo 29, kudhibiti ubora wa chakula, dawa na Vipodozi.

xvi. Kufuatilia mwenendo wa magonjwa ya mlipuko na kutuma taarifa Wizara ya afya.

xvii. Kuhimiza na kusimamia Kaya 913 kuchimba, kujenga na kuboresha vyoo na kuweka vibuyu chirizi.

Shughuli zote hizo zilighariimu **Tzs**. **543,725,193.38.**

Aidha, upatikanaji wa dawa umekuwa mzuri **(90-95%)** kwani baadhi ya dawa muhimu kama vijiua sumu (antibiotics), dawa za malaria, dawa za maumivu na dawa zingine na baadhi ya vitendanishi na vifaa vya maabara vilipatikana kutoka katika Bohari Kuu ya dawa (MSD).

***Usafishaji na Mazingira***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Usafi wa mazingira kwa kufagia ulifanyika katika barabara zipatazo 72, masoko 6 na stendi 3.

ii. Jumla ya mifereji 56 ya maji ya mvua katika kata 09 ilizibuliwa.

iii. Kiasi cha tani 2,520 za taka ngumu kutoka kwenye kaya, taasisi, makampuni na vizimba zilizolewa, kusafirishwa na kutupwa kwenye dampo.

iv. Kufyeka nyasi maeneo ya wazi 09 na kando kando ya barabara na sehemu za wazi kudhibiti mazalia ya mbu, wadudu na wanyama hatari.

v. Vikundi vitatu (03) vya usafi wa mazingira vilisimamiwa ili kutekeleza majukumu yao ya usafi katika maeneo yao ya kimkataba.

vi. Kiwanda cha Majengo elution plant kilikaguliwa na mmiliki kupewa notisi ya kufanya marekebisho ya mifumo ya kulinda mazingira hususan kufunika shimo la maji taka, kukamilisha vyoo na mabafu, kukamilisha mtambo wa kulipulia (blasting room) pamoja na kukamilisha stoo ya madawa, kukarabati sakafu kwa kutumia saruji isiyopitisha maji na kuweka alama za usalama .

vii. Ukaguzi ulifanyika katika kata ya Kitaji kuhusu utiririshaji wa maji taka ambapo jumla ya watu 4 walitozwa faini **Tzs. 300,000.00** kwa kosa la kutiririsha majitaka.

viii. Kuitisha na kusimamia kikao cha wadau wa madini ujenzi ili kuwapa elimu ya mazingira, ulipaji ushuru na suala la mchakato wa kuanzisha eneo moja la kuchukua madini hayo litakalosimamiwa na Halmashauri (eneo la Mugaranjabo).

ix. Usimamizi wa uzingatiwaji wa masuala ya mazingira katika kuanzishwa kwa kituo cha uchenjuaji dhahabu cha Ndg. Julius Ryoba Orindo na kituo cha Manyawa Group (zamani kikiitwa Lyabonde Group) katika eneo la SIDO kata ya Nyakato kwa kushirikisha kamati ya Mazingira ya Kata (WDC) ulifanyika.

x. Kuainisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vyoo 40 katika shule za msingi, vyoo 18 katika shule za sekondari na vyoo 9 vitakavyojengwa katika maeneo ya wazi ikiwa ni sehemu ya mradi wa mfumo wa majitaka chini ya MUWASA.

xi. Ukaguzi wa kiwanda cha maji cha Serengeti, kiwanda cha samaki cha MFPL, viwanda 13 vya kuchenjua dhahabu (vat leaching na elution plants), hoteli 06, Beach (fukwe zilizoendelezwa) 07, Vituo vya mafuta (petrol stations) 07, Garage 03, viwanda vya mikate 03, Mradi wa Ufugaji samaki wa Jeshi (27 KJ) Lake side na Kiwanda cha nguo cha Mutex ulifanyika.

Shughuli zote hizo zilizogharimu **Tzs**. **79,151,899.01.**

***Elimu ya Msingi***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Ukaguzi na ufuatiliaji wa maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji ulifanyika katika shule za msingi za Mwisenge ‘B’, Mwisenge ‘A’, Kigera ‘A’, Kigera ‘B’, Kwangwa, Nyarigamba “A”, Mshikamano ‘A’ na ‘B’, Kamunyonge ‘A’, na ‘B’, Mtakuja ‘A’ na ‘B’ na Rwamlimi ‘B’.

ii. Kusimamia uandikishaji wa wanafunzi wa Darasa la Awali kwa mwaka 2019 ambapo wanafunzi 2,232 (Wav - 1,099 na Was - 1,133) waliandikishwa hadi Desemba, 2018 sawa na asilimia 49 ya maoteo ya ya wanafunzi 4,586 (Wav - 2,217 na Was 2,369).

iii. Kusimamia uandikishaji wa wanafunzi wa Darasa la Kwanza kwa mwaka 2019 ambapo wanafunzi 2,350 (Wav - 1,135 na Was - 1,215) waliandikishwa hadi Desemba, 2018 sawa na asilimia 49 ya maoteo ya ya wanafunzi 4,797 (Wav - 2,357 na Was 2,440).

iv. Kuendesha mitihani ya darasa la nne katika shule 54 na darasa la saba katika shule za msingi 52.

v. Kufuatilia matumizi ya fedha ruzuku ya Elimu Bila Malipo kwa shule za msingi 38.

vi. Kupokea na kugawa vitabu vya Mtaala mpya Darsa la I hadi IV ambapo vitabu vya kiada vilivyopokelewa ni 19,375, vya Hadithi ni 9,176 na Miongozo kwa ufundishaji kwa walimu ni vitabu 912.

vii. Kukamilisha ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule ya msingi Kamunyonge ‘B’, kukamilisha ujenzi wa shule shikizi ya Bukanga na kuanza ujenzi wa shule shikizi za Rwamlimi na Nyabisare.

viii. Kuwezesha wanafunzi stadi za umahili wa kuhesabu, kusoma na Kuhesabu (KKK).

ix. Kushiriki shughuli maalum ya Uchaguzi wa wanafunzi kuingia kidato cha kwanza 2019 ambapo wanafunzi 3,531 wavulana 1,754 na wasichana 1,777 walifaulu kuingia kidato cha kwanza sawa na asilimia 79.80 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa Taifa wa darasa la Saba 2018.

x. Usimamizi na Ufuatiliaji wa vituo vya **MEMKWA** pamoja na ukaguzi wa ufundishaji kwa kutumia zana.

Shughuli zote zilizogharimu **Tzs. 774,956,316.53.**

***Elimu ya Sekondari***

i. Kusimamia shughuli za ufundishaji na ujifunzaji shuleni katika shule za sekondari 25.
ii. Kuendesha mafunzo kazini kwa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati.
iii. Kufanya maandalizi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 36.
iv. Usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za chakula kwa shule tatu **3** za bweni jumla ya **Tzs. 437,631,933,** fedha za rukuzu (capitation) kwa shule **18** jumla **Tzs. 56,165,838.65** na fedha za fidia ya ada **Tzs**. **89,464,049.30** kwa shule 17 umefanyika.
v. Kusimamia uendeshaji wa mitihani ya Taifa kwa kidato cha IV na Kidato cha II, 2018. Katika shule za sekondari, ambapo Jumla ya watahiniwa 2,197 (Me - 1,307 & Ke - 890) kidato cha IV na watahiniwa 3,443 (Me - 1,870 & Ke - 1,573 ) kidato cha II walifanya mtihani huo.
vi. Kushiriki zoezi la uchaguzi wa wanafunzi wa kidato cha I- 2018 ambapo Jumla ya wanafunzi 3,519 waliofaulu wamechaguliwa wanafunz 2,250 kulingana na uwepo wa vyumba vya madarasa na wanafunzi 1,269 watachaguliwa baada ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 36.
vii. Kusimamia mapokezi ya wanafunzi 589 walioripoti kati ya wanafunzi 778 waliopangwa kidato cha V.
viii. Kushirikiana na shirika la WEI (Bantwana) chini ya mradi wa Waache Wasome katika kutoa elimu ya kutokomeza ukatili wa kijinsia katika shule za sekondari saba (7).

Shughuli zote hizo zilizogharimu **Tzs**. **200,967,483.78.**

***Maji na Udhibiti wa maji taka***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Usimamizi wa ujenzi wa matanki ya kuvuna ya mvua katika shule za msingi za Buhare na Mshikamano.
ii. Usimamizi wa ukarabati wa choo cha soko la Saanane Nyakato, Ofisi kuu ya Manispaa ya Musoma na kupeleka maji ya bomba katika vyoo soko la Saanane na kuingiza kwenye vyoo.
iii. Kusimamia ukarabati wa mfumo wa maji safi na maji taka katika kituo cha Afya Nyasho na Ofisi ya Afisa Elimu Sekondari.
iv. Kusimamia ukarabati wa mfumo wa maji safi katika Shule ya Msingi Mkendo.

v. Kusimamia ujenzi wa mnara wa tanki soko kuu na ufungaji wa mfumo wa maji wa tanki la lita 5,000 pamoja na ukarabati wa mifumo ya maji safi na maji taka.
vi. Kusimamia ukarabati wa mfumo wa maji safi katika Kituo cha Afya Nyasho, zahanati ya Nyamatare na maji taka nyumba ya Mkurugenzi.
vii. Kusimamia ufungaji wa mfumo wa maji safi na maji taka katika kituo cha Afya Makoko kinachojengwa.
viii. Kuandaa ripoti ya matumizi ya fedha za mradi wa maji (RWSSP) na kuzituma Wizara ya Maji na OR-TAMISEMI. Zilizo katika mfumo wa **MIS.**

Shughuli zote hizo zilizogharimu **Tzs**. **27,704,050.00.**

***Maendeleo ya Jamii***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kuhamasisha na kutoa elimu ya uundaji wa vikundi ambapo vikundi 75 vya kijamii vimetambuliwa na kupewa barua ya utambuzi na kuorodheshwa kwenye rejista ya kumbukumbu na kati ya hivyo, vikundi 46 vimefanikiwa kufungua akaunti benki.
ii. Kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto 20,823 wenye umri chini ya miaka 5, wamesajiliwa na kupewa vyeti sawa na asilimia 87.6 kati ya watoto 23,775 waliokadiriwa.
iii. Uhakiki wa vikundi umefanyika kwa vikundi 20 kwa ajili ya kupewa mkopo (vikundi vya wanawake 13 na vikundi vya vijana 7). Aidha, vikundi 20 vyote vilipatiwa mkopo kiasi cha **Tzs. 24,500,000.**00 kati ya **Tzs. 50,000,000.00** zilizotolewa na Halmashauri.
iv. Ufuatiliaji na kuhimiza urejeshaji wa mikopo kwa vikundi vyote vilivyowahi kukopeshwa na Halmashauri kwenye kata zote 16 umefanyika. Kiasi cha **Tzs. 3,339,600.00** kilirejeshwa.
v. Halmashauri kwa kushirikiana na shirika la WEI, wameunda vikundi 50 kwa kata 8 za Makoko, Mwisenge, Buhare, Nyamatare, Iringo, Mwigobero, Nyasho na Bweri na kutoa elimu ya Uongozi, utunzaji wa kumbukumbu na utatuzi wa migogoro kwa viongozi wa vikundi na wawezeshaji wa vikundi.
vi. Halmashauri kwa kushirikiana na jeshi la polisi kitengo cha dawati la jinsia na watoto imetoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia katika chuo cha Musoma utalii na chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare katika maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.
vii. Watoto saba (7) wa mitaani wameunganishwa na familia zao kwa kushirikiana na jeshi la polisi kitengo cha dawati la jinsia na watoto, kati ya hao 1 anatokea Buhare, 2 Nyakato, 1 Kinesi, 1 Makoko na 2 Tarime.
viii. Rufaa za watoto zimetolewa kwenda kulelewa kituo cha jipe moyo watoto 7, Mji wa huruma watoto 2 na Musoma childrens watoto 3.

ix. Kesi 34 za migogoro na matunzo ya watoto zimeripotiwa na kupatiwa ufumbuzi.
x. Kesi 27 za ulinzi na usalama wa mtoto zimeripotiwa na kushughulikiwa ambapo kesi 1 ya ubakaji ipo mahakamani.
xi. Kuwezesha watu 30 wenye ulemavu kuhudhuria maadhimisho ya siku ya watu wenye ulemavu Duniani tarehe 3/12/2018, ambayo kimkoa yalifanyika Wilayani Butiama.

Shughuli zote hizo zilighariimu **Tzs**. **24,971,000.00.**

***Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Wakulima 2,686 wa mazao mbalimbali katika Kata 16 za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma walitembelewa na kupewa ushauri kuhusu kulima kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo cha mazao wanayolima.
ii. Maafisa ugani 10 walipewa mafunzo kuhusu njia bora za kutoa huduma za ugani kwa wakulima.
iii. Wakulima 5, viongozi 24, watumishi 13 na wajasiriamali 23 walishiriki katika maonesho ya kilimo yaliyofanyika kitaifa mkoani Simiyu na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilikuwa mshindi wa kwanza kitaifa na ilitoa mkulima wa kwanza bora kitaifa.
iv. Ufuatiliaji na uratibu wa takwimu za bei za vyakula ulifanyika kila wiki na kupata wastani wa bei katika mwezi, taarifa ya hali ya chakula kila Mwezi iliandaliwa na kuwasilishwa Mkoani.
v. Wataalamu wa ugani ngazi ya Halmashauri walifuatilia utendaji kazi wa wataalamu wa ugani ngazi ya kata mara tatu katika kipindi cha miezi mitatu.
vi. Takwimu za kilimo za kila mwezi na robo mwaka zilikusanywa na kuingizwa katika mfumo wa taarifa za kilimo (Agricultural Routine data System - ARDS) "Web Portal".
vii. Ushauri kuhusu njia mbalimbali za umwagiliaji ulitolewa kwa wakulima 34 katika kata 5(Kwangwa 9, Kigera 8, Nyamatare 7, Kamunyonge 5 na Kitaji 5).
viii. Usimamizi na ufuatiliaji wa kilimo cha nyanya ndani ya kitalu nyumba ulifanyika katika kikundi cha vijana wanaosimamiwa na Shirika la Hope Revival Children's Organization mara 40 na katika kikundi cha Nyakamitu.
ix. Kutoa ushauri kuhusu utekelezaji wa majukumu kwa kuzingatia sheria katika vyama vya ushirika 6.
x. Kuhudhuria na kutoa maelekezo ya kisheria kwenye vikao na mikutano mikuu ya mwaka katika vyama vya ushirika 6.
xi. Vikao 4 vya Bodi za vyama vya ushirika (Musoma, Musoma Municipal, AIC Nyasho na Imara) vilifanyika.

xii. Mikutano mikuu ya mwaka ya vyama 2 vya ushirika (Musoma Urban Teachers na Imara) ilifanyika.

xiii. Kutoa semina ya elimu ya ushirika kupitia mkutano mkuu katika Imara SACCOS na kuwasilisha Waraka wa Mrajis Na. 4 wa mwaka 2018 kwa wanachama wa Musoma Urban Teachers na Imara SACCOS.

Shughuli zote hizo zilizogharimu **Tzs**. **28,669,904.00.**

***Mifugo na uvuvi***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Ukaguzi wa awali wa mifugo 3,882 ulifanyika ambapo mifugo 3,515 iliruhusiwa kuchinjwa na nyama kukaguliwa kwa matumizi ya binadamu. Aidha Halmashauri ilikusanya ushuru wa machinjio kiasi cha **Tzs. 12,840,300.00.**

ii. Utambuzi wa magonjwa, ufuatiliaji, utoaji kinga na tiba ulifanyika kwa mifugo 25,092 katika Kata 16 za Manispaa ya Musoma.

iii. Mifugo 1,187 ilipatiwa huduma mbalimbali (kukata pembe, kwato, meno, midomo na kuhasi) na ushauri juu ya ufugaji bora ulitolewa katika Kata 16 za Manispaa ya Musoma.

iv. Kuingiza takwimu za Mifugo na Uvuvi za kila mwezi na kila robo mwaka katika mfumo wa "Agriculture Routine Data System (ARDS) 'Portal Web' kwa mwaka 2018/19.

v. Ufuatiliaji wa shughuli za ugani zinazotekelezwa na maafisa ugani na Taasisi zisizo za Kiserikali ngazi ya Kata ulifanyika.

vi. Kusimamia na kufuatilia uendelezaji wa zao la ngozi.

vii. Kufanya utambuzi wa mifugo, upigaji chapa ng'ombe, uandikishaji na uwekaji wa kumbukumbu wa ng'ombe 113 katika Manispaa ya Musoma.

viii. Kufanya doria 9 ndani na nje ya Ziwa Victoria na kukamata zana haramu za uvuvi 565 pamoja na kukusanya **Tzs. 5,904,000.00** ikiwa ni mapato yanayotokana na leseni za mitumbwi na ukusanyaji wa samaki.

ix. Kutoa huduma ya ushauri wa ufugaji bora wa samaki kwa wadau 295 (109 ufugaji wa samaki na 186 uvuvi endelevu) katika Kata ya Mkendo, Rwamulimi, Makoko na Nyakato.

Shughuli zote hizo zilizogharimu **Tzs**. **10,111,740.00.**

***Mipango miji na Ardhi***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Hati **255** ziliandaliwa na kuwasilishwa kwa Kamishina Msaidizi wa ardhi kanda ya Simiyu.

ii. Usuluhishi wa migogoro **26** ya wananchi umefanyika.

iii. Viwanja **300** vimeainishwa kwenye ramani ya mipango miji.

iv. Upimaji ( urasimishaji) ulifanyika katika maeneo ya Nyamatare na Kiara.

v. Jumla ya ramani ndogo (*Deed plans*) **272** zimechorwa na kuambatishwa kwenye hati zilizoandaliwa.
vi. Viwanja 14 vilikadiriwa thamani.
vii. Uthamini kwa ajili ya kuhamisha milki wa viwanja 17 ulifanyika.
viii. Uthamini kwa ajili ya kuhuisha hati milki 8 ulifanyika.
ix. Mali za wananchi 6 zimefanyiwa uthamini.
x. Jumla ya michoro 6 katika eneo la Nyamiongo, Rwamlimi Bondeni, Rwamlimi kati, Mshikamano na Nyamatare iliandaliwa na ipo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kupitishwa/kuidhinishwa na Wizara.
xi. Halmashauri kwa kushirikiana na ofisi ya Mkuu wa Wilaya iliotesha jumla ya miche ya miti **250,212** katika eneo la PCI na miche ya miti **20,342** imepandwa katika Taasisi za Serikali na watu binafsi.Halmashauri na Wizara wametembelea na kuibaini Shule ya msingi Mwisenge kama Majengo ya Kihistoria.

Shughuli zote hizo zilighariimu **Tzs**. **19,161,267.00.**

***Ujenzi***

Shughuli zilizotekelezwa ni:-

i. Usimamizi wa ujenzi unaoendelea wa barabara za lami mjini chini ya Programu ya Uboreshaji wa Miji (ULGSP) zenye jumla ya urefu wa **km 9.867** kwa gharama ya **Tzs. 10,803,059,618.54** kwa mchanganuo ufuatao:-
   - Gharama za ujenzi **Tzs 9,930,059,618.54** na Mkandarasi Nyanza Road works Ltd wa Mwanza.
   - Gharama za ushauri na usimamizi (Consultancy and Supervision Services) ni **Tzs 873,000,000.00** na Mtaalamu Mshauri ni Norplan Tanzania Ltd wa Dar es salaam.

ii. Halmashauri iliendelea na ufuatiliaji ili gari la kubebea taka ngumu la tani 10 lililonunuliwa na Mzabuni Hughes Motors (T) Ltd wa USA River Arusha kwa gharama ya **Tzs. 207,546,600.00** ili likabidhiwe kwa Halmashauri.
iii. Katika miradi ya majengo Halmashauri ilipokea jumla ya Ramani thelathini na moja (22) kwa ajili ya kupata vibali vya ujenzi na vibali hivyo vilitolewa kwa wahusika kuendelea na ujenzi.
iv. Usimamizi wa kazi za majengo mbalimbali ya watu binafsi, shule za serikali, vituo vya kutolea huduma za afya ulifanyika.

***Teknolojia ya habari, mawasiliano na uhusiano***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kuratibu na kusimamia waandishi wa Habari katika matukio mbalimbali ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
ii. Uchukuaji na uhifadhi wa matukio muhimu yaliyofanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ikiwa ni uchukuaji wa picha, video na sauti. Jumla ya picha za mnato 558 na video 14 zilichukuliwa.
iii. Uingizaji na uhuishaji wa taarifa katika tovuti umefanyika ambapo jumla ya taarifa mpya 66 zimewekwa katika tovuti. Uandishi wa makala 4 na habari 9 zimeandikwa na kuwekwa katika tovuti ya Halmashauri.
iv. Uratibu wa malalamiko ya wananchi umefanyika. Jumla ya malalamiko 37 yalipokelewa na kupelekwa idara husika kwa ajili ya utatuzi ambapo kati ya malalamiko 37 yaliyopokelewa malalamiko 33 yamekamilika na malalamiko 4 yako katika hatua mbalimbali za utatuzi.
v. Utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA katika idara mbalimbali umefanyika ili kuhakikisha usalama na utendaji kazi wake unakuwa katika hali nzuri.
vi. Kitengo kimehakikisha mifumo ya **GSPP, PLANREP, FFARS, TASAF, EPICOR, HCMIS, BEMIS, GoT-HoMIS, LGRCIS** na **TSA** inakuwa katika usalama pamoja na kuendelea kufanya kazi ipasavyo.
vii. Kitengo kwa kushirikiana na Idara ya Fedha kimehakikisha kuwa vifaa vinavyotumika kukusanya mapato (**POS**) vinakuwa salama na vinafanya kazi ipasavyo.

Shughuli zote hizo zilighariimu **Tzs**. **3,581,500.00.**

***Kitengo cha Sheria***

Shughuli zilizotekelezwa ni zifuatazo:-

i. Kusimamia na kufuatilia kesi za madai zinazoihusu Halmashauri zilizoko mahakamani ambazo ni kesi za madai **41** ambazo zilikuwa katika Mahakama mbalimbali (Mahakama Kuu ya Tanzania – Mwanza, Mahakama ya Wilaya – Musoma, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya – Musoma, Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma, Mahakama ya Mwanzo na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya kazi (**CMA)**. Kati ya kesi **41** kesi **6** ziliamuliwa na Halmashauri kushinda, kesi **35** zinaendelea na kati ya kesi zinazoendelea kesi **4** ziliamliwa miaka ya nyuma na Halmashauri inapaswa kutekeleza amri za Mahakama kwa maana hiyo majalada ya kesi hizo hayajafungwa kwa sababu amri za Mahakama hazijatekelezwa.

ii. Usimamizi wa sheria mama na sheria ndogo, ambapo katika kusimamia sheria, Kitengo kimeshiriki katika zoezi la ukaguzi wa ujenzi holela, zoezi la ulipaji wa ada ya usajili wa magari ya biashara na kudhibiti mifugo inayozururra ovyo. Katika mazoezi yote hayo jumla ya kiasi cha **Tzs. 3,120,000.00** zilikusanywa ikiwa ni ada ya usajili wa magari ya biashara, faini kwa waliobainika kujenga bila vibali na gharama za ukamataji wa mifugo. Pia wafanyabiashara ndogondogo ndani ya stendi ya mjini na maeneo mengine yasiyo rasmi waliondolewa.

Shughuli zote hizo zilizigharimu **Tzs**. **8,912,000.00.**

***Kitengo cha Ununuzi na ugavi***

Shughuli zilizotekelezwa na kitengo ni zifuatazo:-

i. Kupokea na kujadili Taarifa ya majadiliano kuhusu huduma ya unyonyaji wa majitaka katika Manispaa ya Musoma.
ii. Kupokea na kujadili matumizi ya fedha za Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa ajili ya kununua mabati ya kuezekea vyumba vya madarasa na fedha za mapato ya Ndani (Own Source) kwa ajili ya ununuzi wa saruji na usafirishaji.
iii. Kupokea na kujadili na kuridhia kwa njia ya mzunguko (Circular Resolution) – Taarifa ya majadiliano kuhusu huduma ya unyonyaji wa majitaka katika Manispaa ya Musoma.
iv. Kufanya manunuzi kwa ajili ya ujenzi wa matanki ya maji katika shule za msingi za Buhare na Mshikamano, ujenzi wa karo la kuchinjia kuku katika soko la Nyasho na ufungaji wa gata za maji katika sekondari ya Nyamiongo na Kituo cha Afya Bweri kwa gharama ya **Tzs. 72,353,397.90.**

Shughuli zilizotekelezwa zilizigharimu **Tzs. 4,619,500.00.**

***Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani***

Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kimetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufuatilia ili kujiridhisha kama mfumo wa udhibiti wa ndani unafanya kazi na kufuatilia hoja za nyuma.
ii. Kufanya ukaguzi kwa ajili ya ufanya tathimini kwa shughuli zilizofanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 kwa kufanya ukaguzi wa nyaraka (Transaction Audit) na ukaguzi wa miradi ya maendeleo
iii. Kuandaa taarifa za ukaguzi wa ndani kwa robo 2 za mwaka

Shughuli zote zilizigharimu **Tzs. 4,518,000.00.**

***Kitengo cha nyuki***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

Kuhamasisha wafugaji nyuki 10 na vikundi 3 kukagua mizinga yao ya nyuki na kuifanyia usafi

***Uchaguzi***

Kuandaa na kufanya uchaguzi wa Serikali za mitaa mwaka 2019 na Jumla shilingi **230,414,220.52** zilitumika katika kuendesha uchaguzi huo.

***Mhe. Mwenyekiti,***

Halmashauri katika kutekeleza mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kufikia tarehe 31, Desemba 2019 ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

| Na. | Changamoto | Suluhisho |
|---|---|---|
| 1. | Upungufu wa watumishi hususani katika Idara ya Afya, Elimu Msingi na Sekondari | Kufuatilia vibali vya ajira na kuajiri watumishi |
| 2. | Kutotolewa kwa fedha kwa ajili ya utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na upungufu wa fedha za uendeshaji wa Halmashauri. | Kuendelea kuomba Serikali kutoa fedha kwa mujibu wa mpango kazi wa Halmashauri. |
| 3. | Upungufu wa vitendea kazi. | Kununua vitendea kazi |

## 4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

***Mhe. Mwenyekiti,***

Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha **2020/2021** yamezingatia Miongozo na Sera mbalimbali kama vile:-

i. Dira ya Taifa (Vision) 2025
ii. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.
iii. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015.
iv. Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu.
v. Uwezo wa Halmashauri wa kukusanya mapato yake.
vi. Masuala mtambuka.

***Mhe. Mwenyekiti,***

Kwa kuzingatia mambo muhimu yaliyotajwa hapo juu Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha **2020/2021** umekuwa na vipaumbele katika maeneo muhimu yafuatayo:-

i. Kuboresha Elimu ya Msingi na Sekondari kwa kuimarisha taaluma na kuhakikisha tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati/meza kwa shule za msingi na sekondari linatatuliwa.
ii. Kuongeza miundombinu kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya na kuongeza ufanisi wa huduma zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya.
iii. Kuboresha huduma za kiuchumi ikiwemo kukamilisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.
iv. Kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vyetu wenyewe.
v. Kulipa fidia ya mali za wananchi katika maeneo yaliyotolewa yatakayotwaliwa na Halmashauri.
vi. Kulipia deni la mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.

***Mhe. Mwenyekiti***,

Mpango na Bajeti unaowasilishwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2020/2021 na kisha kujadiliwa na Baraza la Madiwani ni kwa ajili ya kuhudumia wakazi **179,962 (Me- 84,908 & Ke- 95,054**) kwa mujibu wa maoteo ya Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2019.

**Mapato tarajiwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2020/2021** Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inatarajia kupata jumla ya **Tzs. 27,635,211,675.97** kutokana na mapato ya ndani (OS), ruzuku ya matumizi mengineyo, mishahara na miradi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

***A: Mapato ya ndani***

Mapato ya ndani (Own sources) ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ya kwa mwaka wa fedha **2020/2021** yanatarajiwa kupatikana kutokana na vyanzo vifuatavyo:-

| NA | CHANZO | MAKISIO |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa machinjio | 48,816,000.00 |
| 2 | Ushuru wa stendi ya mabasi na taxi | 119,718,000.00 |
| 3 | Ushuru wa huduma | 316,350,000.00 |
| 4 | Leseni za vileo | 15,128,000.00 |
| 5 | Ada ya usajili wa magari mdogo | 16,350,000.00 |
| 6 | Ushuru wa Masoko | 10,008,000.00 |
| 7 | Ushuru wa samaki na dagaa | 170,040,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 8 | Kodi ya vibanda vya Biashara | 419,581,000.00 |
| 9 | Ada ya maombi ya zabuni | 13,500,000.00 |
| 10 | Ada ya nyumba za kulala wageni | 50,162,400.00 |
| 11 | Ada ya usajili wa vyombo vya majini | 25,000,000.00 |
| 12 | Leseni za biashara | 240,080,000.00 |
| 13 | TIKA/NHIF/USER FEE | 198,791,202.88 |
| 14 | Ushuru wa vyoo vya kulipia na Bafu | 27,840,000.00 |
| 15 | Ada ya usajili wa Hospitali bianafsi | 15,000,000.00 |
| 16 | Michango mingine kwenye shule za Sekondari | 699,957,000.00 |
| 17 | Adhabu ya ukiukwaji wa sheria | 6,000,000.00 |
| 18 | Ushuru wa maeneo ya kuoshea magari | 4,562,500.00 |
| 19 | Mapato Mengineyo | 500,000.00 |
| 20 | Ada ya vibali vya ujenzi | 6,000,000.00 |
| 21 | Ada ya kukodisha ukumbi | 6,000,000.00 |
| 22 | Ushuru wa minara ya simu | 30,543,840.00 |
| 23 | Ada za shule za sekondari (kidato cha V & VI) | 87,080,000.00 |
| 24 | Ushuru wa madini ujenzi | 89,425,000.00 |
| 25 | Ada ya kuzoa taka ngumu | 65,271,000.00 |
| | **Jumla** | **2,681,703,942.88** |

Makadirio ya mapato ya ndani kwa mwaka **2020/2021** ni **Tzs. 2,681,703,942.88** ni sawa na ongezeko la asilimia **20.52** ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2019/2020 ambayo yalikuwa ni **Tzs. 2,131,421,000.00**

***B: Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC)***

Halmashauri inatarajia kupata ruzuku kwa ajili ya shughuli ambazo siyo miradi ya maendeleo kiasi cha **Tzs. 703,619,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:-

| NA | IDARA | MAKISIO |
|---|---|---|
| 1 | Utawala na Utumishi | 59,063,000.00 |
| 2 | Kilimo & mifugo | 6,807,000.00 |
| 3 | Elimu Msingi | 310,908,000.00 |
| 4 | Elimu Sekondari | 249,151,000.00 |
| 5 | Afya | 69,928,000.00 |
| 6 | Ujenzi | 7,762,000.00 |
| | **Jumla** | **703,619,000.00** |

***C: Mishahara***

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2020/2021 inakisia kutumia **Tzs. 21,668,305,920.00** kulipia mishahara ya watumishi **1,524** kama ifuatavyo:-

| NA | KASMA | MAKISIO |
|---|---|---|
| 1 | Kilimo, Umwagiliaji na ushirika | 236,641,920.00 |
| 2 | Mifugo na Uvuvi | 407,510,640.00 |
| 3 | Afya | 2,891,813,760.00 |
| 4 | Utawala | 2,681,703,942.00 |
| 5 | Elimu msingi utawala | 128,164,520.00 |
| 6 | Elimu msingi | 9,731,153,200.00 |
| 7 | Elimu sekondari | 5,594,771,760.00 |
| 8 | Ujenzi | 243,516,000.00 |
| | **Jumla** | **21,668,305,920.00** |

***D: Miradi ya Maendeleo***

***Mhe. Mwenyekiti,***

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha **2020/2021** inatarajia kupokea kiasi cha **Tzs. 3,259,933,109.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

| NA | CHANZO | MAKISIO |
|---|---|---|
| 1 | Elimu Bila Malipo | 1,745,954,999.97 |
| 2 | Ruzuku ya uendeshaji wa shule | 333,515,000.00 |
| 3 | Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo | 36,616,000.00 |
| 4 | Mfuko wa pamoja wa Afya (HSBF) | 403,505,813.00 |
| 5 | Mpango wa kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini miaka 5 (U5BR) | 7,500,000.00 |
| 6 | Mpango wa Maendeleo kwa shule za Msingi (PEDP) | 50,000,000.00 |
| | **Jumla** | **3,259,933,109.97** |

Aidha Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani inatarajia kutumia **Tzs. 678,350,296.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo.

***Mhe. Mwenyekiti,***

Mchanganuo wa shughuli za maendeleo zitakazotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umeainishwa kwenye jedwali lifuatalo:-

| Sekta | Shughuli | Kiasi cha fedha |
|---|---|---|
| ***Mapato ya Halmashauri (Own Sources)*** | | |
| Mipango, Takwimu | Kulipia deni la Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 120,000,000.00 |
| | Kuandaa Mpango na Bajeti wa Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022 | 9,582,351.00 |

| | | |
|---|---|---|
| na Ufuatiliaji | Kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa michoro kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa kituo cha mabasi Bweri na Mialo ya Nyarusurya na Makon ko | 70,000,000.00 |
| | Ukarabati wa soko Kuu na jengo la kupumzikia wasafiri | 34,180,371.00 |
| Ujenzi | Kufungua barabara za kata za pembezoni na kulipa fidia wananchi | 20,000,000.00 |
| Elimu ya Msingi | Kuchangia ujenzi wa madarasa Shue za Msingi | 40,000,000.00 |
| | Ukarabati wa nyumba za walimu | 30,000,000.00 |
| Elimu ya Msingi | Kutengeneza madawati 50 kwenye shule 39 za Msingi | 10,000,000.00 |
| Elimu ya Sekondari | Kutengeneza viti na meza 500 kwenye shule 15 za Sekondari | 30,000,000.00 |
| Mipango Miji na Ardhi | Kulipa fidia kwa wananchi mbalimbali ambao ardhi yao imetwaliwa/itatwaliwa kwa matumizi ya shughuli za serikali | 50,000,000.00 |
| Maendeleo ya Jamii | Kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu | 169,587,574.00 |
| Afya | Kuchangia ujenzi wa jengo la OPD la zahanati kwenye kata ya Kamunyonge | 20,000,000.00 |
| | Kuchangia ujenzi wa choo zahanati ya Iringo | 10,000,000.00 |
| | Kuchangia ujenzi wa jengo la OPD la zahanati kwenye kata ya Mshikamano | 20,000,000.00 |
| Kilimo | Kushiriki maonesho ya nanenane kitaifa Mkoani Simiyu | 20,000,000.00 |
| Mifugo na uvuvi | Kukarabati machinjio ya Bweri | 10,000,000.00 |
| | Kufanya operation za kupambana na Uvuvi na kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya uvuvi | 5,000,000.00 |
| | Kushiriki maonesho ya nanenane kitaifa Mkoani Simiyu | 10,000,000.00 |
| | **Jumla ndogo** | **678,350,296.00** |
| ***Programu ya Utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka 5(U5BR)*** | | |
| Maendeleo ya Jamii | Kufanya ufuatiliaji na kugawa vifaa vya kuandikisha na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka mitano kwenye vituo vyote 36 vya uandikishaji | 7,500,000.00 |
| | **Jumla ndogo** | **7,500,000.00** |
| ***Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo (CDCF)*** | | |
| Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | Kuchangia miradi kupitia Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF) | 36,616,000.00 |
| | **Jumla ndogo** | **36,616,000.00** |
| **Mpango wa Maendeleo kwa elimu ya Msingi (PEDP)** | | |
| Elimu Msingi | Kujenga vyumba vya madarasa kwenye shule za msingi | 50,000,000.00 |
| | | **50,000,000.00** |

| | | |
|---|---|---|
| ***Elimu bila malipo (Free Education)*** | | |
| Elimu Msingi | Kutoa Ruzuku ya uendeshaji wa shule za msingi 39 za Serikali | 173,178,000.00 |
| | Kutoa Ruzuku ya madaraka kwa walimu wakuu 40 wa shule za msingi za Serikali na waratibu elimu kata 16 | 139,200,000.00 |
| | Kutoa Ruzuku ya chakula kwenye shule 3 za msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum za Mwembeni “B”, Mwisenge “B” na Nyarigamba “A” | 286,236,000.00 |
| Elimu sekondari | Kutoa Ruzuku ya uendeshaji wa shule za sekondari 18 za Serikali | 160,337,000.00 |
| | Kutoa Ruzuku ya madaraka kwa walimu wakuu 18 wa shule za sekondari za Serikali | 54,000,000.00 |
| | Kutoa Ruzuku ya chakula kwenye shule 3 za sekondari za bweni za Musoma ufundi, Mara na shule ya wasichana ya Songe | 1,006,020,000.00 |
| | Kutoa Ruzuku ya fidia ya ada kwa wanafunzi wa shule za sekondari 17 | 260,498,999.97 |
| | **Jumla ndogo** | **2,079,469,999.97** |
| ***Mfuko wa pamoja wa Afya (HSBF)*** | | |
| Afya Tiba | Kununua dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara | 40,712,781.00 |
| | Kufanya matengenezo ya vifaa tiba vilivyopo kwenye vituo vya afya na zahanati | 3,585,000.00 |
| | Kuimarisha huduma za mama na mtoto kwa kununua dawa na vitendea kazi | 24,086,346.00 |
| | Kununua dawa na vifaa tiba kwa ajili ya huduma za dharura | 14,369,216.00 |
| | Kuimarisha mfumo wa chanjo kwa ajili ya watoto wachanga | 17,755,000.00 |
| | Kununua vifaa kwa ajili ya matibabu ya watoto chini ya miaka 5 | 12,850,000.00 |
| | Kununua dawa na vifaa tiba kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza kama malaria, VVU, Kifua kikuu n.k | 20,135,300.00 |
| | Kuzuia magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama kisukari, moyo n.k | 2,800,000.00 |
| | Kudhibiti magojwa yanayosumbua kama vile ugonjwa macho, kichocho n.k | 3,163,673.00 |
| | Kuimarisha usafi wa mazingira ya vituo na usafi kwa ujumla | 1,272,940.00 |
| | Kuimarisha kitengo cha ustawi wa jamii, huduma kwa | 6,470,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | ajili ya wasiojiweza, wazee na makundi maalumu kwenye jamii | |
| | Kulipa stahiki mbalimbali za watumishi wa afya, kuwaendeleza kimasomo na kuzingatia maslahi ya watumishi | 16,089,943.00 |
| | Kuimarisha bodi za afya, kamati za vituo na usimamizi wa huduma za Afya, uandaaji wa mipango usimamizi wa fedha, mifumo ya afya na mafuta ya magari | 48,974,698.00 |
| | Kusimamia uendeshaji wa ofisi ya mganga mkuu, vituo vya afya na zahanati, kulipa bili za maji na umeme | 5,625,000.00 |
| | Kufanya matengenezo ya magari ya Idara zikiwemo gari za wagonjwa na kusambaza chanjo | 12,325,000.00 |
| | Kuhamasisha jamii kutumia huduma za afya hasa masuala ya lishe, jamii kujiunga na mfuko wa afya ya jamii na kujikinga na magonjwa | 5,766,103.00 |
| | **Jumla ndogo** | **403,505,813.00** |
| | **Jumla Kuu** | **3,259,933,109.00** |

## 5.0. HITIMISHO

***Mhe. Mwenyekiti,***

Naomba kutoa shukrani za pekee kwa watumishi wote walioshiriki kuandaa Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

***Mhe. Mwenyekiti,***

Naomba sasa nitoe rai kuwa Baraza la Madiwani ipitie, ijadili na kutoa mapendekezo kwenye rasimu hii ili hatimaye iweze kujadiliwa na kuidhinishwa na Baraza la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

***Mhe. Mwenyekiti,***

Naomba kuwasilisha.

Fidelica Myovella
***KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA***
***HALMASHAURI YA MANISPAA***
***MUSOMA***